BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,004,055,092/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SERIKALI** yasema hakuna tishio la usalama Loliondo




UKURASA 11

# Nipashe

Jumamosi Juni 11, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580973
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Ajali tatu eneo moja zilivyoua watu 20



UKURASA 2

Wananchi wakiangalia mabaki ya gari aina ya Toyota Coaster lenye namba za usajili T542 DQV lililogongana na lori la mizigo kwenye mteremko wa Changarawe, eneo la Mafinga wilayani Mufindi mkoani Iringa jana na kusababisha vifo vya watu 20. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## SABAYA ACHOMOKA KESI YA PILI

UKURASA 2



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akizungumza na mawakili wake, Mosses Mahuna na Fauzia Mustapha, kabla ya kuachiwa huru katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha jana. **PICHA: ALLAN ISACK**

UKURASA WA 5

## PROFESA JAY ATOKA MUHIMBILI BAADA YA KULAZWA SIKU 127

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, aliyelazwa kwa siku 127 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili...

## Rais Samia akemea migogoro fedha miradi ya dini

UKURASA 2

MICHEZO YANGA SC YAMFUATA AZIZ KI IVORY COAST =UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akikata utepe kuzindua rasmi Msikiti wa Jami Ul Istiqama, mjini Bukoba, mkoani Kagera jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Istiqama nchini Seif Ali Seif (wa tatu kulia), Sheikh Mkuu wa Tanzania Mufti Abubakar Zubeir bin Ally (wa tatu kushoto), Kaimu Balozi wa Oman hapa nchini, Dk. Salim bin Saif Al Harbi (wa pili kushoto) na (wa nne kushoto) ni Mjumbe wa Jumuiya ya Istiqama, Nassoro Ali Seif. **PICHA: IKULU**

# Ajali ilivyoua watu 20

**Na Francis Godwin**, IRINGA

WATU 20 wamefariki dunia na wengine saba kujeruhiwa katika ajali iliyohusisha lori aina ya scania na Coaster eneo la Changarawe mjini Mafinga Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa jana alfajiri.

Ajali hiyo imehusisha lori aina ya Scania lenye namba za usajiri T 736 AAE na Coaster yenye namba za usajili T542 DQV.

Wakizungumza na Nipashe kwenye eneo la tukio jana, baadhi ya mashuhuda, akiwamo John Kyando na Kefa Sanga, walisema kuwa baada ya ajali, walishuhudia idadi kubwa ya watu waliolazwa chini baada ya ajali hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mafinga, Dk. Victor Msafiri, alisema kuwa ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu 19 ambavyo vilitokea eneo la tukio na majeruhi mmoja alipoteza maisha wodini wakati akipatiwa matibabu.

Alisema kuwa majeruhi wanaendelea kupata matibabu na baadhi ya miili ya marehemu imeshatambulika na wengine wanaendelea kutambuliwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kubainisha kuwa dereva wa lori anashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Kamanda Bukumbi alisema kuwa kabla ya ajali ya Coaster kwenye mteremko huo mkali, kulikuwa na ajali ya lori lililoanguka majira ya saa sita usiku wa kuamkia jana.

Aliendelea kusimulia kuwa Coaster iliiligonga lori na kupinduka na kusababisha vifo vya watu saba papo hapo na majeruhi 16.

Kamanda Bukumbi alisema vifo zaidi katika ajali hiyo vilisababishwa na lori ambalo lilifeli breki na kuwagonga na kuwaua majeruhi 12 waliokuwa wametolewa kwenye Coaster na kulazwa kando ya barabara kuu ya Iringa-Mbeya wakisubiri kukimbizwa hospitalini.

Kwa mujibu wa Kamanda Bukumbi, ajali hiyo imehusisha magari matatu yakiwamo malori mawili na basi dogo hilo aina ya Coaster lililokuwa linatoka Dar es Salaam kwenda Mbeya.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule, akizungumza na wafiwa na Majeruhi katika Hospitali ya Wilaya ya Mufindi, alisema Serikali itaendelea kuwasaidia majeruhi hao na kuwa miili ambayo bado haijatambuliwa, itapelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa ili kuhifadhiwa kutokana na chumba cha kuhifadhi maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Mufindi kuwa kidogo.

Hiyo ni ajali ya pili kutokea eneo hilo na kusababisha vifo vya watu wengi tangu ajali iliyohusisha lori na basi la Majinja kwenye eneo Mei 13, 2015 iliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 50.

## Wajumbe wa bodi TPDC wateuliwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Nishati, Januari Makamba, amewateua wajumbe wanane wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Petroli (TPDC).

Uteuzi huo umekuja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kumteua Balozi Ombeni Sefue kuwa mwenyekiti wa bodi hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Waziri Makamba iliyotolewa jana, wateule ni Ruth Zaipuna, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB na aliwahi kuwa Mkaguzi wa Hesabu za PriceWaterhouseCoopers na Ofisa wa Fedha Standard Chartered.

Wengine ni Dk. Natu Mwamba ambaye ni Mhadhiri Mwandamizi katika Shule Kuu ya Uchumi, Chuo Kikuu cha Dar Salaam na amewahi kuwa Naibu Gavana Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Taarifa hiyo ilimtaja mwingine ni Musa Makame ambaye ni Mshauri Mwelekezi katika sekta ya mafuta na gesi na aliwahi kuwa Ofisa Mwandamizi wa Biashara katika kampuni ya Equinor (zamani Statoil) na kabla ya hapo alikuwa Makamu wa Rais (Fedha na Utawala) katika kampuni ya Wentworth (zamani Artumas).

Mpambika Chiume ambaye ni mshauri mwelekezi kwenye sekta ya mafuta na gesi ambaye aliwahi kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya PanAfrican Energy na Mkuu wa Masuala ya Biashara wa Kampuni ya Ophir Energy na pia kama Msimamizi wa Miradi Kenya na Seychelles.

Waziri Januari pia amemteua Protace Ishengoma ambaye ni Mwanasheria Mbobezi wa Sekta ya Mafuta na Paul Makanza ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC).

Makanza pia ni Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI) na Makamu Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF).

Pia, Dismas Fuko ambaye ni Mshauri Mwelekezi wa Miradi ya Nishati hasa kwenye uchambuzi wa kifedha na alikuwa Mkurugenzi wa Masoko na Uwekezaji wa TPDC na Balozi Kallaghe ambaye ni Mkufunzi wa Chuo cha Ulinzi cha Taifa na aliwahi kuwa Msaidizi wa Rais Ikulu na kwa nyakati tofauti alikuwa Balozi wa Tanzania nchi ya Uingereza, Canada na Cuba.

# Samia akemea migogoro fedha za miradi ya dini

**Na Waandishi Wetu,** BUKOBA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka waumini wa dini ya Kiislamu kuacha tabia ya kuibua migogoro wanapopewa miradi mbalimbali inayoingiza fedha.

Alitoa kauli hiyo jana mjini Bukoba mkoani Kagera alipofungua msikiti wa Jumuia ya Istiqaama uliojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Oman.

Rais Samia alisema katika maeneo mengi inapokuwapo miradi kwenye misikiti, huibuliwa migoro inayotokana na kugombania fedha.

"Kwenye maeneo mengine huibuka mafarakano endapo kuna maduka kwenye eneo la msikiti bila kujua sadaka inayopatikana hapo inatakiwa ifanye ukarabati wa miundombinu ya msikiti," alisema.

Rais aliongeza kuwa nyumba za ibada ni sehemu ya kujenga uhusiano wa amani na upendo na kuwa na itikadi ya imani.

Alisema ujenzi wa nyumba za ibada huleta hamasa kwa taasisi nyingine kujenga nyumba kubwa kwa ajili ya imani ya maisha.

Msikiti huo wa kisasa pia una maeneo ya maduka saba ambayo yataingiza kipato ambacho Rais Samia alitaka kisiwe chanzo cha ugomvi kwa waumini hao.

Rais Samia pia aliwakumbusha waumini hao umuhimu wa kushiriki Sensa ya Watu na Makazi ifikapo Agosti 23 mwaka huu.

Alisema sensa inatoa fursa kwa serikali kutambua idadi ya wakazi wake ili ifahamu namna ya kutoa huduma za maendeleo.

"Wananchi mjitokeze ifikapo Agost 23, mwaka huu kuhesabiwa na hii itasaidia kutoa fursa kwa serikali kupanga mipango sahihi na kujua idadi gani ya watu ilionao," alisema.

Akitoa salamu kwa waumini wa dini ya Kiislamu na viongozi wa serikali, Mufti wa Tanzania, Aboubakary Zubery, alikemea vitendo vya mauaji ya watu.

Sheikh Zubery alisema hakuna dini inayoruhusu mtu kumuua mwenzake wala kumvunjia heshima kwa namna yoyote.

"Nchi yetu ni yenye amani na upendo, inapotokea vitendo vya kujiua na kuuana kwenye familia kwa maudhi ya mke na mume ni dhambi," alionya.

Aliongeza kuwa viongozi wa dini wana nafasi ya kusemea jambo hilo na kulimaliza kwa kushirikiana na viongozi wa serikali.

Mwakilishi wa Serikali ya Oman, Dk. Salim bin Harbi, alisema kazi ya Jumuiya ya Istiqaama nchini siyo kujenga msikiti pekee, bali inafanya miradi yote ikiwamo ya elimu na afya kama sehemu ya ushirikiano.

Mwakilishi wa Jumuiya ya Istiqaama nchini, Sheikh Seif Ali Seif, alisema kuna matawi 21 kwa Tanzania bara na Zanzibar na ujenzi wa msikiti huo ulianza mwaka 2019.

Rais Samia jana alimaliza ziara yake ya siku tatu mkoani Kagera baada ya kutembelea kiwanda cha sukari cha Kagera, kufungua mradi wa maji wa Kyaka-Bunazi na kushiriki sherehe za kufungua msikiti mkubwa uliopo mjini Bukoba.

●**Imeandaliwa na Richard Makore na Restuta Damian**

# Sabaya achomoka katika kesi ya pili

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imemwachia huru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (pichani) na wenzake sita katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 kwa kuwa hati ya mashtaka ilikuwa na upungufu wa kisheria.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akisoma hukumu hiyo jana mahakamani huko, Hakimu wa Mahakama hiyo, Dk. Patricia Kisinda, alisema katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi ya mwaka 2021 ilikuwa na washtakiwa saba na walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matano.

Alisema mashtaka matatu yalikuwa yakimkabili mshtakiwa wa kwanza (Sabaya) na mengine mawili yaliwahusu washtakiwa wengine sita katika shauri hilo.

Hakimu Kisinda alisema upande wa Jamhuri ulipeleka mashahidi 13 na vielelezo 12 na upande wa utetezi ulikuwa na mashahidi wanane na kielelezo kimoja.



Alisema mahakama hiyo ilipitia ushahidi wa pande zote mbili na kuuchambua kwa kina kulingana na matakwa ya kisheria na kujiridhisha kwamba ushahidi uliotolewa mahakamani haujaweza kuthibitisha mashtaka hayo pasipo shaka yoyote.

"Ushahidi ulikuwa umegubikwa na maswali mengi yalikosa majibu ya kisheria kupitia ushahidi uliotetwa. Pia, mahakama imeona hati ya mashtaka ilikuwa na upungufu wa kisheria, hivyo imesababisha washtakiwa kutokukutwa na hatia katika makosa hayo.

"Kutokana na sababu hizo mahakama imewaachia huru washtakiwa wote kutokana na makosa waliyoshtakiwa mahakamani na kama kuna upande haujaridhika na uamuzi wa mahakama, mnaweza kukata rufani ndani ya siku 30," alisema Hakimu Dk. Kisinda.

Baada ya kusomwa kwa hukumu hiyo, Ole Sabaya alisikika akisema kuwa kwa mara nyingine Mwenyezi Mungu ametenda muujiza huku akimshukuru mke wake, Jesca Thomas, kwa kumwombea.

Ndugu, jamaa na marafiki wa Sabaya, akiwamo mama yake mzazi na mke wake, pia walionekana wakiwa na furaha baada ya kushinda kesi kwa mara nyingine. Sabaya pia alishinda rufani dhidi ya hukumu ya kesi ya kwanza aliyokuwa ametiwa hatiani na kutakiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani.

# Serikali yasema hakuna tishio la usalama Loliondo

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania na wananchi wa Loliondo kupuuza upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu wasiolitakia mema Taifa kuhusu eneo la Hifadhi ya Loliondo lililoko Tarafa ya Loliondo na badala yake waendelee kuisikiliza serikali.

"Kilichotokea si uhalisia, hakuna tishio lolote, wale wameenda msituni kuweka alama katika eneo ambalo liko mbali sana kijiji cha karibu kipo umbali wa kilomita nane.

"Wananchi waendelee na shughuli zao, wasisikilize upotoshaji unaofanywa na baadhi ya watu wasiopenda maendeleo ya nchi hii, hakuna mapambano yoyote, hakuna askari yeyote aliyekwenda huko kijijini kutishia amani," Majaliwa alisema bungeni jana alipotoa kauli ya serikali kuhusu taarifa zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii kuhusu eneo la Hifadhi ya Loliondo wilayani Ngorongoro mkoani Arusha.

Alisisitiza kwamba wananchi watulie na serikali haina lengo la kumhamisha mtu, vijiji vyote 14 vitaendelea kuwapo.

Alisema serikali inaamini wale wanaofanya hamasa za vurugu katika eneo la Loliondo wataacha mara moja kufanya hivyo ili kuwaacha wananchi waendelee na shughuli zao. "Wanapaswa kufahamu kwamba wanapeleka usumbufu mkubwa kwa kina mama, wazee na watoto, Serikali ipo macho dhidi yao.

"Ninataka niwaambie serikali ipo macho na hatutamwonea mtu yeyote.

Wananchi watulie, hakuna shughuli yoyote ya kumhamisha mtu, hatuna lengo la kumhamisha mtu kwenye eneo la Loliondo.

"Lile eneo ni letu sote na tutaliratibu vizuri. Alama zinazowekwa ni wigo wa kuonyesha mipaka ambayo kwa pamoja tutaitumia kulinda na kulihifadhi eneo lile," alisema.

Waziri Mkuu alisema shughuli za maendeleo zinazofanywa na serikali katika eneo lenye vijiji ni pamoja na uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa majosho na mabakuli ya kunyweshea mifugo.

Alisema watendaji wa Wizara ya Maji na Wizara ya Mifugo na Uvuvi wapo katika maeneo hayo wakiendelea na kazi.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema video iliyosambaa mtandaoni ikionyesha wananchi wenye silaha za jadi waliokusanyika kuonyesha kuna tatizo, haina uhalisia.

Katika taarifa yake, Waziri Mkuu alisema chanzo cha kusambaa kwa video hiyo, ni baada ya watumishi wa serikali waliokuwa wanakwenda kuweka mipaka wakiwa katika Kijiji cha Ololosokwani, ndipo wananchi wakaitana viongozi wao wakatengeneza video na kuzisambaza.

"Walitengeneza video lakini hakuna kundi la askari wala mtumishi yeyote walifanya majaribio wazirushe kuonyesha Loliondo kuna tatizo na ndiyo maana unaona kwenye video hakuna askari yeyote.

"Video iliyorushwa ilikuwa na lengo la kutengeneza picha mbaya ya nchi yetu ndani na nje ya nchi, lakini kimsingi hakukuwa na mapambano yoyote, hakuna askari aliyekwenda kujjijini kutishia kwa kuwa kwenye mpango hakuna kijiji kinaondolewa, mtu anaondoka, mwenyewe.

"Tunasema haya ili kuondoa dhana mbaya dhidi ya serikali kwamba inataka kuvunja vijiji 14, kuwaondoa wafugaji. Baada ya alama kukamilika serikali itakaa na viongozi kuandaa mfumo bora wa matumizi," alisema.

Akizungumzia kuhusu Tarafa ya Ngorongoro, Majaliwa alisema tayari kaya 293 zenye watu 1,497 zimeshajiandikisha kwa ajili ya kuhama kwa hiari kutoka Hifadhi ya Ngorongoro na kuhamia katika Kijiji cha Msomera kilichoko Wilaya ya Handeni mkoani Tanga ili kupisha uhifadhi endelevu wa Hifadhi ya Ngorongoro.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliishauri serikali kuwachukulia hatua za kisheria wote waliohusika na upotoshaji huo.

"Pamoja na elimu kutolewa mara kwa mara, upotoshaji bado unaendelea kwa sababu hakuna hatua za kisheria zinazochukuliwa dhidi ya wanaofanya upotoshaji huo, hasa wale walioko hapa nchini," Spika Tulia alisisitiza.


## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**DAVID N MALIWA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC 873 CYP.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **IRI/IRI/RB/228602/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**IMANI LAMECK KIRENGA**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No S.2421/0089Mwaka 2017 Shule ya Sekondari STAR HIGH SECONDARY SCHOOL, kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa polisi: **DOD/DOD/RB/113716/2022.**

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc, 5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama, New Bagamoyo Road, P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania | Telephone +255 22 277 4577 | Fax: +255 22 277 4559 | Email: info@victoriafinance.co.tz | Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | JELEMIA LIHO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-MAJENGO MADIBIRA | HOLLINESS AND RESPISHERS COMPANY | 25 - 06 - 2022 |
| 2. | YUSUPH NYAGAWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-CHALISUKA MADIBIRA | HOLLINESS AND RESPISHERS COMPANY | 25 - 06 - 2022 |
| 3. | DANIEL NDELE | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO-MAGUNGULI MAHANGO MADIBIRA | HOLLINESS AND RESPISHERS COMPANY | 25 - 06 - 2022 |
| 4. | HURUMA KIMKANGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO-MAGUNGULI MAHANGO MADIBIRA | HOLLINESS AND RESPISHERS COMPANY | 25 - 06 - 2022 |
| 5. | BARAKA HANGO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – MAJENGO MAHANGO MADIBIRA | HOLLINESS AND RESPISHERS COMPANY | 25 - 06 - 2022 |
| 6. | VERONICA IMBYANDUMI KIMARO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIGOGO MBUYUNI | JOFORTE AUCTION MART | 25 - 06 - 2022 |
| 7. | GRACE MAGOBEKO ODUNGA | GARI | TOYOTA PREMIO – T 631 DKA | JODAC PROFESSIONALS LTD | 25 - 06 - 2022 |
| 8. | RADSON MASAWE | PAGALE | MKATABA WA MAUZIANO – MABWAWANI CHALISUKA MADIBIRA | HOLLINESS AND RESPISHERS COMPANY | 25 - 06 - 2022 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

**216896802**

SGS

## INVITATION FOR BIDS

**Dear APPLICANTS ON THE 6TH/06/2022 THIS ADVERT WAS PUBLISHED KINDLY IGNORE THE PREVIOUS PUBLICATION AND APPLY AS PER THE REQUIREMENTS OF TODAYS ADVERT .**

| | REF NUMBER | REG # | TYPE | MAKE & MODEL | YOM | LOCATION / BID FORM DEPOSIT TZS25,0000/= | CONTACT |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TZ_VEH0000085 | MC812BER | MOTOR CYCLE | BAJAJ BOXER BM150 (Red) | 2016 | Dar es salaam-SGS Office, Kinondoni **ECO Bank a/c # 7045002612** SGS Superintendence | Anna Moshy - 0756454968 |
| 2 | TZ_VEH0000084 | MC913BEN | MOTOR CYCLE | BAJAJ BOXER BM150 (Red) | 2016 | | |
| 3 | TZ_VEH0000078 | T997DFR | MOTOR VEHICLE | TOYOTA RAV4 (COLOR BLACK) | 2005 | | |
| 4 | TZ_AA/VEH0015 | T724AEY | MOTOR VEHICLE | MITSUBISHI PICK UP, DC, 4X4 | 2003 | Mwanza-SGS Office, Mkuyuni **ECO Bank a/c # 7045002609** African Assay | Alex Nairo - 0755754882 |
| 5 | TZ_AA/VEH0042 | T609APK | MOTOR VEHICLE | MITSUBISHI FUSO TRUCK | 1995 | | |
| 6 | TZ_AA/VEH0045 | - | CRANE | TRUCK CRANE | - | | |
| 7 | TZ_AA/VEH00XX | - | FORK LIFT | FIAT FORK LIFT | - | | |

216897802

Vehicles are sold on **"AS IS WHERE IS BASIS"** and viewing can be done at various locations indicated above during normal working hours 10:00 AM to 16:00 PM from **8th June to 16th June 2022**. Interested bidders must pay a non-refundable fee by Depositing TZS. 25,000 ECO Bank a/c # 7045002612 for Dar and TZS. 25,000 ECO Bank a/c # 7045002609 for Mwanza and submit the slip attached with your bid in our tender boxes located at the reception for Dar es salaam and Mwanza.

Bids should be submitted, not later than **18th June, 2022 by 10.00 AM.**

For more details please contact us via **+255 756454968 for Dar es salaam / 0755 755754882 for Mwanza or alternatively e-mail us at TZ.Procurement@sgs.com**

WWW.SGS.COM WHEN YOU NEED TO BE SURE SGS

# Serikali kuendelea kusaidia wabunifu

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imeahidi kuendelea kusaidia wabunifu wanaojitokeza katika kubuni vifaa tiba vya afya kwa watoto wachanga na magonjwa mbalimbali ili kupunguza vifo vyao na wajawazito.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Seif Shekhalage, alisema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa maonyesho ya vifaa tiba vikiwamo vya watoto wachanga vilivyobuniwa na wabunifu wakiwamo wanaosimamiw na Taasisi ya Afya Ifakara.

Shekhalage alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Taasisi ya Afya Ifakara kwa kuwa imekuwa na msaada mkubwa katika kubuni na kutengeneza vifaa tiba ambavyo vimekuwa vikisaidia wagonjwa na kutumika baadhi ya hospitali.

Alisema serikali haina budi kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wabunifu wazawa kwa sababu kazi zao zinaleta manufaa makubwa nchini.

"Kwanza kabisa taasisi yetu hii ya sayansi na teknolojia, ina jukumu kubwa la kuratibu mambo ya ubunifu kwa hiyo wabunifu wanaanzia hapa wakishakamilisha ubunifu wao ziko taasisi ambazo zimepewa jukumu la kusajili, kuangalia ubora ufanisi.

"Taasisi hii ikishavipitisha na kuona kama vinakidhi ubora, kunakuwa hakuna shida vitaingia sokoni na vinasajiliwa kama vingine vinavyotoka nje," alisema.

Msajili wa Vifaa Tiba na Vitendanishi kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Rehema Maliki, aliwataka wabunifu wote wenye lengo la kubuni vifaa tiba kufika ofisini kwao ili kupata elimu na kuongezewa uelewa.

Kaimu Mkurugenzi wa Uvumbuzi wa Teknolojia wa COSTECH, Dk. Gerald Kafuku, alisema tume hiyo itaendelea kusaidia wabunifu kupata huduma na kuwataka baadhi ya wafanyakazi kupunguza urasimu.

"Maonyesho haya ya leo (jana) yatakwenda kuweka mambo yote sawa ambayo awali yalikuwa kikwazo kwa wabunifu na kwa bahati nzuri tupo na kiongozi kutoka Wizara ya Afya, hivyo niwahakikishie Watanzania kuanzia leo hakutokuwa na vikwazo tena," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Taasisi ya Afya ya Ifakara, Masoud Mnonji, aliishukuru Serikali ya Uswisi kupitia ubalozi wake nchini kwa kuwapa ufadhili wa fedha ambazo zimewasaidia katika kufanikisha miradi hiyo.

Wabunifu wakiwamo wanaotoka Kituo cha Kibunifu ya Afya Ifakara walipata wasaa wa kuonyesha kazi zao ikiwa ni pamoja na kifaa cha kuwasaidia watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya muda.




Wadau kutoka Taasisi ya lishe ya Global Alliance for Improved Nutrition (GAIN), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Taasisi ya Chakula ma Lishe (TFNC), wakiangalia sampuli ya mashine ya kuweka virutubishi kwenye unga wa mahindi, walipotembelea kwa ajili ya kuikagua katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), eneo la akiba jana. Mashine hiyo, imebuniwa na mwanafunzi wa taasisi hiyo, Lucas Sabule, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya kutaka vyuo vya teknolojia kubuni mashine za aina hiyo ili kupunguza utapiamlo nchini. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wataka tathmini mpya kodi ya gari la kifahari Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Zanzibar imesema kampuni ya mifuko Turky inayomilikiwa na mfanyabiashara na Mbunge wa Mpendae (CCM), Toufky Salum Turky, imewasilisha maombi ya kutaka tathmini ya deni la kodi ya gari ya kifahari aina ya Benzi la Sh. milioni 308.5 ifanyike upya baada ya maombi ya msamaha kukataliwa mara mbili na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Naibu Kamishna wa TRA Zanzibar, Juma Bakary Hassan, alisema maombi hayo wamepokea baada ya wahusika kupewa siku saba wawe wamelipa baada ya maombi ya msamaha wa kodi kukataliwa na waziri.

"Baada ya kuwapa siku saba wawe wamelipa deni la kodi wametuletea maombi wakitaka kufanyike tathmini upya ya kiwango cha deni lakini pia mwanzo waliomba walipe kidogo kidogo kwa awamu tatu," alisema.

Naibu Kamishna huyo alisema wahusika baada ya maombi ya msamha wa kodi kukataliwa na waziri, wanatakiwa kulipa kiasi hicho cha kodi kama kilivyokuwa kimefanyiwa tathmini kutokana na thamani ya gari dola za marekani 2014,668.7 kabla ya gari kutolewa kwa dhamana ya bodi ya shirika moja la bima nchini Januari mwaka huu.

Alisema tathmini ya kiwango cha kodi wanachotakiwa kulipa kilifanyika baada ya wahusika kuwasilisha wenyewe nyaraka za thamani ya gari kabla ya kutolewa katika Bandari ya Malindi baada ya kuingizwa nchini na kampuni ya Kimataifa ya Uwakala wa Mizigo ya (WU1) HT Motors Group Limited United Kingdom kwa kushirikiana na Kampuni ya Wakala wa Mizigo ya ZARA Freight Forwarders ya Malindi Zanzibar. Waziri Saada alisema msamaha wa kodi unatakiwa kutolewa kwa wawekezaji wakati wa ujenzi wa mradi na sio baada ya mradi kukamilika na kuanza uzalishaji kama ilivyojitokeza kwa kampuni hiyo na kampuni ya usafi ya Vigors Celea visiwani Zanzibar.

# Watoto na vijana waathirika wakubwa dawa za kulevya

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imesema waathirika wakubwa wa dawa hizo ni vijana wa kuanzia umri wa miaka 15 hadi 40, jambo linalohitaji ushirikiano wa jamii kupambana nalo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), George Simbachawene, amesema dawa za kulevya zinazozalishwa viwandani mwaka 2021 zilikamatwa tani 1.13 za heroine ikiwa ni kiasi kikubwa kuwahi kukamatwa kwa mwaka mmoja katika historia ya nchi.

Hayo yalisemwa jana na viongozi hao baada ya kuwasilishwa bungeni kwa taarifa ya hali ya dawa za kulevya mwaka 2021.

Akijibu maswali ya waandishi wa habari mara baada ya waziri kutoa taarifa jana Dodoma, Kamishna Jenerali wa mamlaka hiyo, Gerald Kusaya, alisema hadi kufikia Desemba mwaka jana kulikuwa na waraibu wa dawa za kulevya 909,902 waliojitokeza kupata tiba katika hospitali za wilaya na mikoa nchini.

"Tuna waraibu 10,600 wanaokwenda kupata matibabu katika vituo 15 vilivyopo, wengi ni vijana wa umri wa miaka 15 hadi 40, ni wachache sana wanavuka hapo, ni nguvu kasi ya taifa na ndiyo wako huku, hata ukienda Sober Houses. Wanaongezeka na ambao hatujawatambua wanakadiriwa zaidi ya 500,000 ila wengi wanatumia kwa siri, tunaendelea na jitihada kuwasaidia," alisema.

Awali, katika taarifa yake, Waziri Simbachawene alisema bangi na mirungi zimeendelea kuwa tatizo kubwa nchini na kwamba mwaka 2021, jumla ya tani 22.74 zilikamatwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 72 ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020.

Alisema ukamataji huo ulihusisha jumla ya watuhumiwa 9,484, huku mirungi iliyokamatwa kwa kipindi hicho ikifikia tani 10.93 zikihusisha watuhumiwa 1,395. Alisema dawa za kulevya za kiwandani zilizokamatwa ni mara tatu ya kiasi kilichokamatwa mwaka 2020 na kwamba cocaine zilikamatwa tani 811.30.

"Kwa mara ya kwanza katika historia ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini, shehena kubwa ya jumla ya kilo 430.77 za dawa za kulevya aina ya methamphetamine inayotengenezwa na kemikali bashirifu ilikamatwa, ikihusisha watumumiwa tisa raia wa Iran," alibainisha.

Simbachawene alisema serikali inaendelea kufuatilia mwenendo wa uingizaji na matumizi ya methamphetamine pamoja na kemikali bashirifu ambazo hutumika kutengeneza dawa hizo.

"Tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuwapo nchini pamoja na juhuda za udhibiti zinazofanywa na serikali... tunaendelea kupanua wigo wa matibabu kwa waraibu ambao hadi Desemba mwaka jana huduma zinapatikana kwenye vituo 15 vya kutolea tiba kwa waraibu wa heroine vilivyosajili watu 15,650.

"Serikali imeendelea kufanya usimamizi katika nyumba 44 za upataji nafuu (sober house) nchini, nyumba hizi huanzishwa na kuendeshwa na asasi za kiraia na serikali," alisema.

Kuhusu kudhibiti mashamba ya bangi, Kusaya alisema yanalimwa porini huku akitolea mfano wa shamba kubwa lililopo Kilosa umbali wa saa 10 kwa kutembea kwa miguu kulifikia.

Kamishna huyo alisema sheria inaruhusu kutaifisha mashamba yanayokutwa yanalima bangi na kwamba watafanya hivyo ikiwa ni jitihada za kukomesha kilimo hicho.

Kuhusu matumizi ya shisha inayodaiwa kuongezwa dawa za kulevya, alisema hadi sasa inahesabiwa kama kiburudisho lakini wanafanya uchunguzi kuhusu madai kuwa inawekewa dawa za kulevya, huku akiwataka watumiaji kutathmini faida na hasara zake.

## Profesa Jay atoka Muhimbili baada ya kulazwa siku 127

**Na Romana Mallya**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, aliyelazwa kwa siku 127 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimkabili, ameruhusiwa kwenda nyumbani baada ya afya yake kuimarika.

Mbali ya kuwa msanii, Profesa Jay amekuwa mbunge kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2015 akilitumikia Jimbo la Mikumi, Mkoa wa Morogoro kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa MNH, Aminiel Aligaesha, aliithibitishia Nipashe jana kuruhusiwa kwa msanii huyo kwenda nyumbani baada ya afya yake kuimarika.

"Msanii Joseph Haule, maarufu Profesa Jay, aliruhusiwa kwenda nyumbani jana (juzi) baada ya afya yake kuimarika, amelazwa hapa Hospitali ya Muhimbili kwa muda wa siku 127," alisema.

Mdogo wa msanii huyo, Black Rhyno, kupitia ukurasa wake wa Instagram jana aliandika: "Watu wanaweza kudhani kwa kuwa Profesa Jay ametoka hospitalini, basi atakuwa yupo tayari nyumbani, mtu akiwa amekaa hospitalini muda mrefu hauwezi kutoka moja kwa moja ukaenda nyumbani.

"Bado kuna uangalizi ambao anatakiwa aendelee kuupata. Siyo kwamba yupo nyumbani kwake ila ametoka hospitalini na yupo sehemu (bila kuitaja) anapatiwa uangalizi maalum na siyo nyumbani kwake kama watu wanavyodhani."

Profesa Jay alianza shughuli za muziki mwaka 1989 na alijiunga na kundi la Hard Blasters Crew (HBC) 1994 na mwaka 1995, Jay na HBC walishinda tuzo ya kundi bora la Hip Hop nchini.

Jay na HBC walitoa albamu ya kwanza iitwayo 'Funga Kazi' mwaka 2000, ambayo ilileta mapinduzi makubwa ya muziki wa Hip Hop nchini na ndani yake kuna nyimbo kama 'Chemsha Bongo' na 'Mamsapu' ambazo zilichangia kufanya muziki wa Bongo Flava kupewa heshima.

Mwaka 2001 aliamua kuwa msanii binafsi na alitoa albamu yake ya kwanza iitwayo 'Machozi Jasho na Damu' na ndani yake kukiwa na wimbo wa 'Ndio Mzee' na 'Piga Makofi' na 'Bongo Dar es Salaam'.

Ilipofika mwaka 2003 alitoa albamu ya pili ijulikanayo kama 'Mapinduzi Halisi' ikiwa na nyimbo mbalimbali zikiwamo 'Zali la Mentali', 'Msinitenge,' na 'Promota Anabeep' na mwezi Januari 2006 alitoa albamu ya tatu 'J.O.S.E.P.H' na mwaka jana aliachia kibao kingine kijulikanacho kama 'Baba'.

# 1,500 wakubali kuhama Ngorongoro kwa hiyari

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kuwa jumla ya kaya 293 zenye watu 1,497 zimeridhia kuhama ndani ya Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA) hadi jana usiku na watajengewa nyumba, kulipwa fidia, kusafirishwa na kupewa eneo lenye ukubwa wa ekari tatu.

Alibainisha hayo bungeni jijini hapa jana alipotoa taarifa kufuatia video iliyosambaa mitandaoni na kuzua taharuki jana ikonyesha wananchi wa jamii ya Kimasai wenye silaha za jadi, wakidai kutokukubali kuondoka kwenye eneo lao.

Alisema wananchi hao wanahamia Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga na kwamba bado hawajaanza kuhamishwa kwa kuwa serikali inajipanga kuhakikisha mazingira mazuri ya wao kuishi.

"Mazingira hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya vyumba vitatu hadi sasa tumeshajenga nyumba 103, zimekamilika kwa asilimia 100 na kila nyumba iko kwenye eneo la ekari tatu, linalomwezesha mkazi huyu kufanya shughuli nyingine hata kuweka boma la mifugo.

"Pia tumewatengea eneo la malisho ambalo wataendesha shughuli zao za malisho, tumewajengea majosho na maeneo ya kunywesha maji kazi inaendelea, tumechimba visima hadi sasa tuna vitatu vinatoa maji ya kutosha.

"Wananchi hao wakienda Kijiji cha Msomela wakitaka kulima tumewatengea eneo la kilimo fursa ambayo haipo Ngorongoro... tumeshajenga shule ya msingi yenye vyumba saba, sekondari vyumba vinane na zote zimekamilika, tumekarabati zahanati ya kutibu wagonjwa wa kijiji hicho na jirani ambacho wanakaa wafugaji. "TAMISEMI kwenye kata ile imejenga kituo cha afya, sasa Watanzania wenzangu serikali inafanya haya yote tunataka nini tena? Tumefanya tathimini ya nyumba zao siku ya kuhama tutapeleka mabasi, malori ya kubeba samani, mifugo na tutawalipa fidia ya nyumba zao," alisema.

Waziri Mkuu alisema fedha imeshatolewa na kilichobaki ni utekelezaji ili kulinda hali ya eneo hilo kwa maslahi mapana ya nchi.

"Nani ameumia kwenye zoezi hili? Wapi tumevunja nyumba? Nani anahamishwa kwa nguvu? Kwanini wapotoshaji wanaingia na kufanya haya?" alihoji.

Alisema watakaopewa nyumba, pia watapewa hati miliki na kwamba kati yake 179 wameshapigwa picha kwa ajili ya nyaraka hizo na zitaendelea kwa wote waliokubali kuondoka kwa hiyari.

"Mpaka tunafikia hatua hii tumeshafanya tathimini ya watoto watakaojiunga darasa la awali 250, darasa la kwanza 181 na sekondari 36. Zoezi hili siyo endelevu na maeneo mengine ni kwa ajili ya Ngorongoro... isije ikajenga mazoea kutaka wajengewe nyumba," alisema.

Alisema wamefanya vikao na madiwani, viongozi wa kimila, watendaji wa kata, vijiji na wadau wa eneo hilo kwa ajili ya kutoa elimu.

"Kimsingi eneo la Ngorongoro idadi ya mifugo, nyumba zilizojengwa kiholela na watu imeongezeka sana, tukiacha ikiendelea bila kutoa elimu na kupunguza, utalii utakuwa ndoto kwa Tanzania.

"Vikao vyote tulivyoviendesha tulikuwa tunajadiliana namna ya kupunguza idadi ya watu, mifugo na ujenzi holela, vimeshirikisha wananchi hadi wakaomba walete maoni yao, niliwapa mwezi mzima na wiki iliyopita walikuwa hapa (Dodoma) viongozi na wawakilishi 60 nilikutana nao," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitoa ufafanuzi kuhusu taarifa zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii kuhusu eneo la Hifadhi ya Loliondo, wilayani Ngorongoro, mkoani Arusha, bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Sekta binafsi imesahaulika katika nyongeza mshahara'

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

CHAMA cha Wafanyakazi wa Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri (TUICO) kimemshauri Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, kuiangalia sekta binafsi kwenye ongezeko la kima cha chini cha mshahara baada ya kusahaulika kwa zaidi ya miaka minane ili kwenda sambamba na ongezeko kwa watumishi wa umma.

Mwenyekiti wa TUICO Taifa, Paul Sangeze, alipaza kilio hicho wakati akizungumza na wajumbe wa baraza kuu la chama hicho mjini Morogoro, akibainisha kuwa wafanyakazi wa sekta binafsi wakiongezwa mshahara watakuwa na furaha na kufanya kazi kwa ari na bidii kubwa.

Kuhusu migogoro ya wafanyakazi, alisema chama hicho kina takriban migogoro 1,400 inayoendelea kutatuliwa katika ngazi mbalimbali za uamuzi na kwamba wingi wa migogoro hiyo unatokana na ukubwa wa chama hicho na aina ya watu wanaowahudumia.

Aliwataka viongozi wa TUICO kuhakikisha migogoro sehemu za kazi inatatuliwa Ili kuiondoa au kupunguza ili kuongeza tija kazini kwa kuwa maeneo ambayo hayana migogoro, wafanyakazi hufanya kazi kwa bidii na kuendelea kuzalisha kwa wingi.

Alihimiza viongozi kusimamia majadiliano na kufunga mikataba ya hali bora sehemu za kazi, hivyo kuhimiza maeneo yote ya kazi kuwa na mikataba ya hali bora ambapo wamefanikiwa kufunga mikataba isiyopungua 80 kwa mwaka 2021, jambo ambalo linaonyesha hatua kubwa kwa wafanyakazi.

Mjumbe wa Baraza la TUICO, Enna Ringo, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza mishahara kwa watumishi wa umma, hali aliyodai itajenga ufanisi na kuongeza tija mahali pa kazi. "Hatuko tayari kuona maadui ndani ya chama chetu sehemu za kazi wanavuruga na kutaka kurudisha nyuma maendeleo yaliyopatikana, tutaendelea kupambana, kujenga mshikamano na kuimarisha chama, tunamshukuru sana Rais wetu," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF anzisheni Ligi ya soka vyuo vikuu

**TIMU** ya Taifa, Taifa Stars, haifanyi vizuri sana kwenye mashindano ya kimataifa na sababu zinaweza kutajwa nyingi sana, lakini ukweli ni kwamba, nchi haina wachezaji bora wanaoweza kuipa mafanikio timu hiyo.

Kwa miaka mingi Stars imekuwa haifanyi vizuri katika mashindano ya timu ya Taifa. Hii inatokana na kukosa Wachezaji wenye uwezo wa kupambana na kuleta matokeo chanya.

Pamoja na klabu kuwekeza kwa wachezaji wao na pia kuanzisha timu za vijana chini ya umri wa miaka 17, lakini mwishowe wengi wao hupotelea sehemu nyingine hasa mashuleni ambako ndio wanakoona wanaweza kupata maisha mazuri baada ya masomo yao.

Sisi tukiwa kama wadau wakuu wa mpira wa miguu Tanzania, tunaona kwamba, huu ni wakati sasa kwa Shirikisho la mpira wa miguu Tanzania (TFF) kuanzisha Ligi ya Wanavyuo.

Ligi hiyo inakuwa ikihusisha vyuo mbalimbali vilivyopo nchini ili kuweza kuibua vipaji vitakavyosaidia timu ya taifa. Kunaweza kusiwe na matokeo ya haraka katika kupata vipaji, lakini tunaamini mbeleni kunaweza kuleta matokeo chanya.

Huu ni ushauri tukiwa kama wadau wa soka, kwani kwa uwepo wa Ligi ya vyuo vikuu tunaamini kabisa tutaweza kutoa wachezaji bora na wa kiwango cha juu kabisa.

Hiyo inatakiwa kufanyika kuanzia vyuo vikuu, vyuo vya kati na vyuo vingine ili wanafunzi waweze kuonesha uwezo wao na baadae kuisaidia timu ya Taifa. Hii pia itawasaidia wanafunzi kujipatia vipato vyao kupitia mishahara na kujikimu kwa namna mbalimbali.

Chuo ambacho kitawezesha timu yake kushinda ligi hiyo, basi TFF waweke utaratibu kwa kushirikiana na bodi ya Ligi kuhakikisha kuwa timu itakayoongoza Ligi iweze kuingia moja kwa moja kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kama ilivyo kwa Ligi Daraja la Pili na la kwanza, uwepo wa Ligi ya vyuo Tanzaia kunaweza kuwa msaada mkubwa kwa soka letu hapa nchini.

Kwa muda mrefu sasa, michezo vyuoni imekuwa ikisahaulika na Wanafunzi wamekuwa wakicheza kama sehemu ya kujifurahisha tu bila kuwa na malengo maalumu au mipango madhubuti ya michezo wanayoshiriki. Na hii tunaona kwamba, inachangiwa sana na kukosa sapoti kutoka kwa mamlaka zinazosimamia michezo nchini.

Ni ukweli usiopingika kuwa vyuo vinabeba vijana wengi wenye vipaji vikubwa katika michezo, hasa mpira wa miguu. Kama TFF itaweza kutumia kundi kubwa kama hili la vijana katika kupata na kuibua vipaji, tunaamini wanaweza kuwa msaada mkubwa zaidi nchini.

Tunaona kwamba, TFF isaidie kusimamia Ligi hiyo ili kutafuta wadhamini na wawekezaji katika timu hizi ili ziweze kujiendesha.

Ni wakati sasa wa TFF kuangalia hili kundi muhimu nchini na kuwasadia hawa vijana ili waweze kuonesha uwezo wao wanapokuwa vyuoni na mara baada ya kumaliza chuo waweze kujiunga na timu mbalimbali nje na ndani ya nchi.


Kwani hii pia itakuwa sehemu ya kupunguza tatizo la ajira nchini, kwani wachezaji wa vyuo ambao watakuwa na mafanikio makubwa zaidi wanaweza kupata ajira kupitia michezo na kujitengenezea fedha nyingi.

Ni matumaini yetu kuwa TFF, Bodi ya Ligi, Wizara inayohusika na vyuo hapa nchini vitakaa chini na kukubaliana kuanza kwa mchakato huo.

Tunaamini baada ya miaka mitatu na kuendelea, tunaweza tukajikuta tuna wachezaji wengi sana wenye vipaji vya hali ya juu hapa nchini ambao watakuwa msaada mkubwa kwa nchi.

Wakati ndio huu, tunaweza kuamua sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ligi yenye pesa ndefu, tatizo viwanja

Na Adam Fungamwangwo

**WAKATI** akitangaza zawadi na bonasi ambazo timu za Ligi Kuu zitapata, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi alibainisha kuwa ligi ya Tanzania Bara inashika nafasi ya pili kwa kuwa na zawadi kubwa kwa washindi kwenye nchi zilizo chini ya Jangwa la Sahara.

Alisema kuwa ukiondoa timu za Afrika Kaskazini, maarufu kama timu za 'Kiarabu', Tanzania inakamata nafasi ya pili ikiongozwa na Afrika Kusini kwa kutoka zawadi kubwa kwenye ligi.

"Pesa zilizotumika kwa zawadi za washindi na bonasi ni shilingi bilioni moja, milioni mia nane, na elfu 20 ambazo timu zote 16 zitapata na kwa utafiti wetu ni kwamba Tanzania inakuwa ni ya pili kwenye Ukanda wa Chini ya Sahara kwa ligi yetu kuwa na zawadi kubwa kwa washindi, ukiondoa ligi za Afrika Kaskazini. Nchi ya kwanza kwenye ukanda huu ni Afrika Kusini na sisi tuko kwenye nafasi ya pili," alisema Kasongo.

Kwenye mchanganuo huo, timu zote 16 zilipata pesa, zingine kama zawadi za ushindi kwa walioshika nafasi tatu za juu, ambazo zimetolewa na wenye haki ya kushusha matangazo, huku zawadi za bingwa hadi nafasi ya tatu zikitolewa na wadhamini wa Ligi Kuu.

Kwa mujibu wa Bodi ya Ligi, Bingwa msimu huu atapata jumla ya Sh. Milioni 600, kiasi cha Sh. Milioni 500 ikiwa ni bonasi na zawadi ya ubingwa ikiwa ni Sh Milioni 100.

Mshindi wa pili imetajwa kuwa anaondoka na jumla ya Sh. Milioni 300, kiasi cha Sh Milioni 250 ni bonasi na zawadi wa mshindi wa pili ikiwa ni Sh. Milioni 50, wakati mshindi wa tatu yeye ataondoka na Sh. Milioni 255, bonasi ni Sh. Milioni 225, na Sh Milioni 30 ikiwa ni zawadi ya mshindi wa tatu wa Ligi Kuu.

Bodi ya Ligi ilisema mshindi wa nne bonasi yake ni Sh. Milioni 200, wa tano atapata kiasi cha Sh. Milioni 65, wa sita Sh Milioni 60, nafasi ya saba atalamba Sh. Milioni 55, huku timu itakayoshika nafasi ya nane, itaondoka na kitita cha Sh Milioni 50, wa tisa Sh. Milioni 45 na wa 10, atapata Sh. Milioni 40.

Timu itakayoshika nafasi ya 11 bonasi yake ni Sh. Milioni 35, na wa 12. Sh. Milioni 30 na timu ya 13 itapata Sh. Milioni 25.

Timu ya 14 ambazo zitacheza mechi ya mchi mchujo itapata Sh Milioni 20 na timu ya 15 na 16 ambazo zitashuka daraja, zenyewe zitapewa Sh Milioni 10 kila moja.

Tunaipongeza Bodi ya Ligi na Shirikisho la Soka Nchini (TFF) na kuifanya Ligi ya Tanzania kuwa moja kati ya ligi bora Afrika.

Kwanza kabisa ni kwa sababu inaonekana kwenye televisheni, tena mechi nyingi zaidi zikirushwa laivu, lakini pia kuruhusu wachezaji wengi wa kigeni kutoka nje ya nchi kucheza soka Bongo, hivyo mashabiki wa nchi hiyo nao kutazama kwa kutaka kuwaona wachezaji wao jinsi wanavyofanya.

Ni hivi karibuni tumeshuhudia mashabiki kutoka Zambia wakiwasili nchini kuangalia mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga, kwa sababu tu ya kutaka kuwaangalia wachezaji wao ambao pia huichezea timu ya taifa, Clatous Chama na Rally Bwalya.

Nchini Zambia kuna tawi la Simba liitwalo Kitwe Supporters ambalo ndilo lililokuja nchini.

Kuna jamaa yangu mmoja ananiambia kuwa Simba ikicheza nchini humo, mashabiki hujazana kwenye vibanda umiza nchini humo kuiangalia kwa ajili ya wachezaji hao.

Nina uhakika hata wachezaji kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Ghana, Burkina Faso, Uganda, Kenya, Burundi, Rwanda na nyinginezo mashabiki watakuwa wakiangalia kama hao wa Zambia kwa ajili ya kuwaona wachezaji wao wanaocheza soka la kulipwa hapa.

Pamoja na yote hayo, bado kuna tatizo kubwa la viwanja nchini. Hili kama litatatulika, basi nadhani ligi ya Tanzania itapiga tena hatua nyingine kubwa zaidi kutoka hapo ilipo. Na ndiyo kila shabiki wa soka nchini anataka hivyo.

Pamoja na ubora wote wa kuwa na pesa ndefu, bado viwanja vinavyotazamika mechi ikichezwa ni vitano tu ambavyo ni Benjamin Mkapa, Azam Complex, na Uhuru, vyote vya Dar es Salaam, Nyamagana Mwanza na Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera. Kati ya hivyo, vinne ni vya nyasi bandia na kimoja ni cha nyasi asilia. Viwanja vilivyobaki kuna wakati vinakuwa bora, lakini huwa ni kwa muda mfupi tu, baadaye vinachakaa na kuwa vibovu.

Nadhani imefika wakati kama ligi ya Tanzania imekuwa bora na kuvutia wengi, pamoja na kuwa na mkwanja mrefu kwa timu zinazoshiriki pamoja na washindi, basi viwanja navyo viboreshwe.

Inafika wakati mechi ya Ligi Kuu inachezwa unaweza kudhani kama ni bonanza, kwani hakuna ufundi wowote unaoonyeshwa zaidi ya kubutua mbele.

Huwezi kuwapata wachezaji wazuri wa timu ya taifa, kama wachezaji kazi yao ni kupiga mbele na kukimbizana, kisa mpira haukai chini kwa sababu ya uwanja.

## Januari: Gharama za umeme hazijapanda

WAZIRI wa Nishati, Januari Makamba, ameliambia Bunge kuwa bei ya umeme haijapanda nchini na kuzitaka mamlaka zinazohusika kuchukua hatua kwa udanganyifu na upotoshwaji uliofanywa kwenye mitandao ya kijamii.

Waziri Makamba aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya.

Mbunge huyo alitaka kujua kama ni kweli bei ya umeme imepanda kwa sababu kwenye mitandao ya jamii alishuhudia jana kuwapo mabishano kuhusu suala hilo.

Akijibu swali hilo, Makamba alisema mchakato wa kupandisha bei ya umeme ni mrefu na hauwezi kufanywa kwa siri.

Alisema mchakato huo unahusisha Shirika la Umeme (TANESCO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma ya Nishati na Maji (EWURA) na wananchi ni lazima wahusishwe kwenye kutoa maoni. Aliwataka Watanzania kupuuzia taarifa hizo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Busanda (CCM), Bryceson Tumaini, alihoji lini Serikali itapeleka umeme wa REA kwenye vijiji zaidi ya 40 ambavyo havina umeme Busanda.

Akijibu swali hilo, Makamba alisema jimbo hilo lina jumla ya vijiji 83 ambapo kati ya hivyo, vijiji 40 vimefikiwa na miundombinu ya umeme na vijiji 43 havina umeme, hivyo vimeingizwa kwenye mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa pili.

"Mradi wa REA awamu ya tatu mzunguko wa Pili katika Mkoa wa Geita ulikumbwa na changamoto iliyotokana na mkandarasi wa kwanza ambaye ni M/s Samheung Electric Power Co. Limited aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi katika Wilaya za Nyan'wale, Mbongwe na Geita mkoani Geita, kushindwa kuwasilisha dhamana ya kutekeleza kazi (Performance Guarantee) ndani ya siku 28 kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi," alisema.

Waziri huyo alisema hali hiyo ilisababisha wakala kuanza upya taratibu za ununuzi wa mkandarasi wa kutekeleza mradi huo katika Mkoa wa Geita ambapo kampuni ya M/S CRJE-CTCE Consortium ilishinda zabuni hiyo.

"REA na Mkandarasi waliingia mkataba mwezi Januari 2022 wa kutekeleza mradi huu unaotarajia kukamilika mwezi Julai 2023, kwa sasa mkandarasi M/S CRJE-CTCE Consortium anaendelea na utekelezaji wa mradi huo kwa gharama ya Sh. bilioni 25.4 katika Mkoa wa Geita na Busanda itafikiwa," alisema.

# Watumishi 7,600 Afya kupangiwa kazi Julai

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa watumishi 7,612 wa kada mbalimbali za afya kwa mwaka wa fedha 2021/22, watapangiwa vituo vya kazi Julai mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Minza Mjika.

Mbunge huyo alihoji ni lini mtaalamu wa X-Ray katika Hospitali ya Wilaya ya Meatu atapelekwa kwa kuwa tatizo hilo limekuwa la muda mrefu na hospitali hiyo ina miaka 30 pasi na kuwa mtaalamu wa kudumu wa X-Ray.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema: "Katika ajira hizi ambazo tunakamilisha mpango kuanzia Julai watapelekwa vituoni, tutapeleka mtaalamu wa X-Ray kwenye Hospitali hii ya Meatu."

Dk. Dugange alisema serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 inaajiri watumishi 7,612 wa kada mbalimbali za afya, wakiwamo wataalamu wa X-ray.

"Hivyo, Hospitali ya Wilaya ya Meatu itapatiwa mtaalamu wa X-Ray baada ya taratibu za ajira kukamilika," alisema.

Mwezi Aprili mwaka huu, ofisi hiyo ilitangaza nafasi za ajira 9,800 kwa kada ya ualimu na 7,612 kwa kada ya afya, ambapo hadi sasa bado haijatoa orodha ya waliopangiwa vituo vya kazi



Mbunge wa Handeni Vijijini, John Sallu, akiuliza swali kuhusu lini serikali itajenga kipoza umeme kutoka kwenye msongo wa KV 132 Mkata, wakati wa mkutano wa saba kikao cha 42 cha Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango maalum kukabili magugu maji waandaliwa

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, amesema mpango maalum umeandaliwa wa kubainisha maeneo yenye tatizo la magugu maji nchini na kwa sasa wapo katika hatua ya kutafuta fedha.

Waziri Jafo alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini hapa alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asia Halamga.

Mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali katika kuokoa Ziwa Babati kwa kuondoa magugu ambayo yanazidi kukua kwa kasi.

Akijibu swali hilo, Dk. Jafo alikiri Ziwa Babati limekuwa na tatizo hilo sambamba na maeneo mengine na ndiyo maana wameandaa mpango maalum wa kubainisha maeneo hayo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Bernadetha Mushashu, alitaka kujua lini Serikali itahakikisha Mto Kanoni ulioko katika Manispaa ya Bukoba, unasafishwa, kina kinaongezwa na kingo zake zinajengwa.

Waziri Jafo, akijibu swali hilo, alisema serikali tayari imeshachukua hatua muhimu za kudumu za kuondoa tatizo la Mto Kanoni ulioko katika Manispaa ya Bukoba.

"Kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba tayari imeibua mradi wa utunzaji wa Mto Kanoni kupitia mradi wa TACTIC unaotarajia kuanza Januari 2023 wenye gharama ya Sh. milioni 500.

"Lengo la mradi ni kuondoa kero kubwa ya mafuriko ambayo hutokea kila mwaka nyakati za mvua ya masika na huathiri zaidi ya kaya 330," alisema.

Alisema mradi huo utahusisha ujenzi wa maeneo makuu mawili ambayo ni kuongeza kina na upana wa mto na ujenzi wa kingo za mto.

Alisema kwa sasa Serikali imeendelea kuchukua hatua za muda mfupi ambapo Manispaa ya Bukoba kila mwaka hutenga kiasi cha Sh. milioni sita kwa ajili ya shughuli za kusafisha, kupanua na kuongeza kina cha mto kwa kuondoa tope, uchafu na miti.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## NOTISI/TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART,REAL MASTER LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MOSHI | HALIMA JUMA MZUNGU | NYUMBA | MARIAM JUMA MZUNGU | BOMANGOMBE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | HURBERTH BENJAMEN MRINGO | NYUMBA | HURBERTH BENJAMEN MRINGO | MWIKA | 01/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MAIMUNA ABDALAH LEMA | NYUMBA | MAIMUNA ABDALAH LEMA | SHABAHA | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SHAFII SWALEHE MRUMA | NYUMBA | SHAFII SWALEHE MRUMA | PASUA | 04/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NICKSON DEOGRATIAS MKINDI | NYUMBA | DEOGRATIAS MKINDI | KIDIRE | 05/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | BRAYSON EMANUEL NNKYA | NYUMBA | BRAYSON EMANUEL NNKYA | MACHAME | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | BALTAZARI LAURENCE CHUWA | NYUMBA | BALTAZARI LAURENCE CHUWA | SANYA JUU | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PATRICK APOLINARY MTEI | NYUMBA | PATRICK APOLINARY MTEI | BOMANGOMBE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MUSTAPHA RAFAELI KILEO | NYUMBA | MUSTAPHA RAFAELI KILEO | SANJA JUU | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MWIDINI SADIKI RAJABU | NYUMBA | MWIDINI SADIKI RAJABU | SANA JUU | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | ZAKAYO LAZARO MOLLEL | NYUMBA | ZAKAYO LAZARO MOLLEL | KARANSI | 06/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NEEMA SOLOMONI MWANGA | NYUMBA | NEEMA SOLOMONI MWANGA | BOMANGOMBE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | ALLAN BARAKAELI MMARY | NYUMBA | ALLAN BARAKAELI MMARY | SANYA JUU | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | ALEX SABAS SILAYO | NYUMBA | ALEX SABAS SILAYO | MABOGINI | 7/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | REGINA WILIUM MBOWE | NYUMBA | REGINA WILIUM MBOWE | MACHAME | 8/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | KANAEL SAIMON NNKO | NYUMBA | KANAEL SAIMON NNKO | NGARE | 11/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | GLORI OBEDI MUNISI | NYUMBA | REMMY OBEDI MUNISI | SADALA | 12/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | LILIAN FELIS RIMOY | NYUMBA | ROBERTH LUCAS MINJA | URU | 12/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MERCELIA JOSEPH MUNISI | NYUMBA | MERCELIA JOSEPH MUNISI | RAU | 12/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | HELEN HUPHREY SHANGO | NYUMBA | HELEN HUPHREY SHANGO | BOMANGOMBE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | DOMINA MARK MAHAMBO | NYUMBA | OMARI NGUZA | SHABAHA | 13/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PRISCUS ERNEST TARIMO | NYUMBA | SANGIWA MYAHAYA MSANGI | SHABAHA | 13/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | CHRISTOHER ELIUDI MTWEVE | NYUMBA | CHRISTOHER ELIUDI MTWEVE/RAMADHANI MWANSHINGA | MAILISITA | 14/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | FATUMA WILIUM MASSAWE | NYUMBA | ZACHARIA PANIEL YUHANA | BOMANGOMBE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PULKERIA MARTIN MANINGI | NYUMBA | PULKERIA MARTIN MANINGI | KIBOSHO | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | JACKSON JONAS SWAI | NYUMBA | JACKSON JONAS SWAI | BOMANGOMBE | 28/06/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | GODFREY JOSEPH MALLYA | NYUMBA | GODFREY JOSEPH MALLYA | KIBOSHO | 15/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | ATHUMAN SAIDIKI MFINANGA | NYUMBA | ATHUMAN SAIDIKI MFINANGA | KIFARU | 19/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SALIMU DAUD NGOVI | NYUMBA | SALIMU DAUD NGOVI | UCHIRA | 20/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | AWADHI JUMA AMIRI | NYUMBA | AWADHI JUMA AMIRI | KIFARU | 21/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SAMIJI ATHUMAN KIBWEREZA | NYUMBA | SAMIJI ATHUMAN KIBWEREZA | MAKANYA | 22/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 30/06/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | FELISTER MATOKE NYANGWE | NYUMBA | SOPHIA KIBOKO CHACHA | KISEKE-MWANZA | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | NYUMBA | HASSAN BUGANDA KAPOJONGO | USTAWI-MWANZA | 05/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOHN MISELYA SHIGELA | KIWANJA | JOHN MISELYA SHIGELA | BUJINGWA-MWANZA | 04/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | NYUMBA NA KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | IGELEGELE BUGARIKA NA BUJINGWA- | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | DICKSON ANICETH GREEN | NYUMBA | DICKSON ANICETH GREEN | LUKOBE-MWANZA | 07/07/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOSEPH KIGONGO IBAMBASI | NYUMBA | JOSEPH IGONGO IBAMBASI | NYAKATO-MWANZA | 12/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | MANGWE EMMAUEL WAMBURA | VIWANJA VIWILI | MANGWE EMMANUEL WAMBURA | ILALILA-MWANZA | 13/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | KIWANJA | CHRISTOPHER MANGARAYA WAMBURA | BUJINGWA-MWANZA | 14/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | GALVAS NDALUKA MAZURI | BAJAJI (2) NAMBA MC215CAW NA MC 702CCM | GALVAS NDALUKA MAZURI | MWANZA MJINI | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | ALLY KASSIMU NANGOMWA | NYUMBA | ALLY KASSIMU NANGOMWA | BUZA-KIDAGAA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | ALLY SHABAN SELLA | NYUMBA | ALLY SHABAN SELLA | BINGWA-MKURANGA | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | SHABANI OMARI MKWAMA | NYUMBA | SHABANI OMARI MKWAMA | KILUNGULE - KIMARA | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| BUGURUNI | AMANI OMARY NOMBWANI | NYUMBA | AMANI OMARY NOMBWANI | KISARAWE II- KIGAMBONI | 30/06/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | DAMAS MODEST KIRIA | NYUMBA | BENEDICT MICHAEL KAZYOBA | KIBAMBA | 27/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | JENIFER MSHASHU KYAKAYORO | GARI TOYOTA COASTER T473 DQN | JENIFER MSHASHU KYAKAYORO | MAKTABA YA TAIFA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | NYUMBA | IBRAHIM HARUNA MKALIPA | MORINGE-MBAGALA | 29/06/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARIAM SAIDI TUMBO | NYUMBA | DAHIMU KASSIMU CHKWAWA | YOMBO DOVYA-MAKANGARAWE | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ISAYA MELKIOR MBOYA | NYUMBA | ELIZABETH MGONZO | KING'AZI 'B'-KIFURU | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KARIAKOO | LILIAN FRANCIS MBETWA | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 100986,KIWANJA NAMBA 70 KITALU '18' | LEILA FRANCIS KAMA MLEZI WA AMIRI HAMISI IDDI | MAGOMENI | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | KASA MUSSA SELEMANI | NYUMBA | KASA MUSSA SELEMANI | CHANIKA | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ABDALLAH SELEMANI YUSUPH | NYUMBA | ABDALLAH SELEMANI YUSUPH | MAJOHE RADA | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | REGNELSON ESHIMAEL MUNISI | NYUMBA | REGNELSON ESHIMAEL MUNISI | KIVULE-ILALA | 27/06/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ELIPIDIUS DEOGRATIUS MGAYUKI | NYUMBA | ELIPIDIUS DEOGRATIUS MGAYUKI | HOMBOZA-KISARAWE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | MAX AYUBU MBONYE | NYUMBA | MAX AYUBU MBONYE | YONGWE-CHANIKA | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ZAITUNI OMARY JUMA | NYUMBA | ZAITUNI OMARY JUMA | KIVULE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | GILASIO DANIEL SOKA | NYUMBA | GILASIO DANIEL SOKA | MSAKUZI | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BENJAMIN PATRICK MABINZA | NYUMBA | BENJAMIN PATRICK MABINZA | MBEZI MSAKUZI | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | ATHUMANI HASSANI HEMEDI | NYUMBA | ATHUMANI HASSANI HEMEDI | ULONGONI 'B' -GONGOLAMBOTO | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | CHRISTOPHER BERNAD KASWALALA | NYUMBA | CHRISTOPHER BERNAD KASWALALA | MALAMBA MAWILI-MSIGANI | 05/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | NAHAL ALLY LIPWAI | NYUMBA | NAHAL ALLY LIPWAI | KONGOWE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | GEORGE JAPHET NDENGA | NYUMBA | GEORGE JAPHET NDENGA | KINYEREZI | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | JAMILA KONDO GEMA | NYUMBA | JAMILA KONDO GEMA | KIPAWA- KIPUNGUNI | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | TABU JANETH JULIUS SEDA | NYUMBA | BRAITI SANGA | MAJOHE MJI MPYA | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | NYUMBA | ABDULHMAN RAJABU MAHABA | ZINGIZIWA | 27/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | NASHON RANGE ROTENTE | NYUMBA | NASHON RANGE ROTENTE | MBONDOLE | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OBEDI ZIHIRWADI MSINGA | NYUMBA | OBEDI ZIHIRWANI | KONGOWE-KIBAHA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | EVALYNE PAULO SAITERU | NYUMBA | EVALYNE PAULO SAITERU | BONYOKWA | 04/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | OMARY SAIDI MNEMBWE | NYUMBA | OMARY SAIDI MNEMBWE | KIBAHA MAILI MOJA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | JUMA SHABANI MAGAZI | NYUMBA | JUMA SHABANI MAGAZI | MTAA WA KILIMAHEWA MAILIMOJA WILAYA YA KIBAHA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | DOTO HARUN MSUYA | NYUMBA | DOTO HARUN MSUYA | MTAA WA TANGINI MAILIMOJA WILAYA YA KIBAHA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | ALPHANI JAFARI JUMA | NYUMBA | ALPHANI JAFARI JUMA | MIEMBE SABA 'B' KIBAHA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | TIMOTHY LUCAS MANYAMA | NYUMBA | TIMOTHY LUCAS MANYAMA | MIEMBE SABA KONGOWE | 12/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KINONDONI | ALEX NAHUMU PALANGYO | NYUMBA | JOSEPH BENJAMIN | MBEZI MTONI | 12/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | MARIAM THADEI HAULE | NYUMBA | MARIAM THADEI HAULE | KIMARA B | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | UPENDO JOSEPH CHALAMBO | NYUMBA | UPENDO JOSEPH CHALAMBO | KIMARA BONYOKWA | 13/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FATUMA ISSA SHIDA | NYUMBA | JUMA SHIGONGO | KIWANGWA | 29/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | STEVEN PIUS MALISA | NYUMBA | STEVEN PIUS MALISA | MTAA WA KIPUNGUNI 'B'-KITUNDA | 05/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | BUMERA LODGE AND CO. LTD | NYUMBA | JOACHIM HERONIMUS MWINGIRA | MTAA WA KIGOGO KATI | 06/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ISMAIL ISSA MICHAEL | NYUMBA | ISMAIL ISSA KASANGA | CHANIKA LUBAKAYA | 14/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | NYUMBA | SEVERINI BONAVENTURA LYIMO | MTONGANI-KUNDUCHI | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ELISANTE BERNADI MRTA | NYUMBA | ELISANTE BERNAD MRTA | SOMANGILA-KIGAMBONI | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | RAMADHANI KITWANA IBRAHIM | NYUMBA | MARIAM KITWANA IBRAHIM | TABATA LIWITI | 04/07/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | FARIDA AYUBU MILLANGA | NYUMBA | FARIDA AYUBU MILLANGA | CHANIKA | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | JUTIA ABDALLAH SANZE | NYUMBA | JUTIA ABDALLAH SANZE | PUGU | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | NYUMBA | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | KISEMVULE | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 30/06/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIWANJA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIVULE | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | BETTY BENSON KAGARUKI | NYUMBA | BETTY BENSON KAGARUKI | MBEZI MSAKUZI | 05/07/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | HUBERT APOLINARY MUSHY | NYUMBA | MWANAISHA IBRAHIM HAJI | MBAGALA KWA KISAUTI - TEMEKE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ABOUBAKER O. HASSAN AND OR SAINECHA | KIWANJA HATI NAMBA 113599 KITALU 'G' TEGETA NA KIWANJA HATI NAMBA 105871 KITALU '12' KIBADA | ABOUBAKER OMAR HASSAN NA SAINECHA ABUBAKARI OMARI | TEGETA NA KIBADA | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | SAIDI AKILIMALI KALILWA | NYUMBA | SAIDI AKILIMALI KALILWA | MWASONGA-KIGAMBONI | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | PAULO GIREMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIREMBE RAWE | KIVULE | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MAIN | DENIS JEREMIAS KIVIKE | NYUMBA | DENIS JEREMIAS KIVIKE | CHANIKA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | GRACE BARNABAS MASUKA | NYUMBA | GRACE BARNABAS MASUKA | USAGARA-MWANZA | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | KIPEJA TIMBER AND GENERAL SUPPLIES | NYUMBA | JOHN TIMOTH PANGANI | IGOMA-MWANZA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | JULIUS KALANGA LAIZER | NYUMBA | JULIUS KALANGA LAIZER | KATA YA ENGUTOTO –MJI PYA MONDULI | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | WORKING MACHINES DODOMA | KIWANJA | RAMADHANI MUSTAPHA IBRAHIM | HOMBOLO BWAWANI | 30/06/2022 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| DODOMA | BARAKA JOHN SEMBEGULI | NYUMBA | BARAKA JOHN SEMBEGULI | CHAMWINO IKULU | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | MAGRETH JOSEPH MASSAWE | NYUMBA | MAGRETH JOSEPH MASSAWE | NZUGUNI-DODOMA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HENRY AGUSTINO SULUO | KIWANJA | HENRY AGUSTINO SULUO | GOMBA ETATE-ARUSHA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | NYUMBA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | KINGORI-ARUMERU | 30/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | NYUMBA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | MOSHONO | 29/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA | MASANJA JAMES WANNA | TERRAT ARUSHA | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | UYACODE VICOBA PROGRAM | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI KNDO 29299-KND/MBR/MWZ/10/2 | UYACODE VICOBA PROGRAM HQ | MAKUBURI UBUNGO | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | CHANIKA MTAA WA ZAVARA | 28/06/2022 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI JOSEPH NYATIENO | CHANIKA BUYUNI | 28/06/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Shamba au Gari ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no .0765999000/ 0754497396 / 0652691275 / 0768672367 / 0713077474 / 0754376493 / 0714939933 / 0718038313 / 07620593303 / 0752360133 / 0754443904 / 0715363537
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216897602


# Pinda atamani kiswahili kitumike kufundishia

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema endapo angekuwa Waziri wa Elimu, angependekeza Lugha ya Kiswahili itumike kufundishia shuleni nchini.

Pinda alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam, alipokaribishwa kutoa maoni yake katika mjadala uliohusu lugha inayopaswa kutumika kufundishia shuleni.

Alisema kuna haja ya kuchukua hatua ili kuienzi lugha hiyo hususani katika kipindi hiki cha kuandaa dira ya maendeleo.

"Lugha ya kiswahili ni tunu na imetusaidia kupata mambo mengi kwa taifa, kwa hiyo tunahitaji kuchukua hatua ili ianze kutumika lakini tukiitazama kisomi, tutakosa mambo mengi. Na kwa wale wa shule binafsi wao tuwaache waendelee na lugha yao ya kiingereza na hata mitihani yao wafanye kwa lugha hiyohiyo, lakini shule hizi za umma wawe na mtihani wao wa kiswahili, hayo ndio maoni yangu," alisema Pinda

"Ni kweli kwamba hizi lugha mbili za Kiingereza na kiswahili ni muhimu sana hasa kwa kuwa sisi kama nchi siyo kisiwa, lakini lugha mojawapo kati ya hizo lazima ibebe uzito kuliko nyingine na mimi maoni yangu ni kwamba kiswahili ndio inatakiwa kubeba uzito zaidi," alisema

Pinda alisema si vibaya lugha nyingine ikiwamo kiingereza zikaendelea kutumika kama lugha za mawasiliano ya kawaida lakini ya kufundishia ndiyo iwe kiswahili.

Mhadhiri mstaafu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (UDSM) Martha Qorro, alisema ni vyema malengo ya kufundisha kwa kutumia lugha ya kiswahili yakawekwa wazi.

Kwa upande wake, Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema ni vyema walimu na wanafunzi wakatumia lugha wanayoielewa vizuri shuleni.

"Lugha ni nyenzo muhimu kufundishia na huzaliwi nayo, unafundishwa kwa hiyo Tanzania kwa hadhi tuliyonayo sasa ni vyema maarifa yapatikane kwa lugha zote mbili, wanaojua kiswahili watumie hiyo na wanaojua kiingereza watumie hiyo,"alisema Prof. Mkumbo.

Mmoja wa walimu wanaofundisha shule za sekondari, Sadick Siza, alisema wanapata changamoto kubwa kuwafundisha wanafunzi wanaowapokea kutoka kwenye shule za msingi zinazofundisha lugha ya kiswahili.

"Mimi kama mwalimu kwa kipindi chote ambacho nimekuwa nikifanya kazi hii ya ualimu, nimeshuhudia kukutana na changamoto kubwa ya kuwabadilisha wanafunzi kwa miaka saba wametumia lugha ya kiswahili kujifunza halafu wanapokuja kidato cha kwanza wanakutana na lugha mpya ya kiingereza, "alisema Siza.

"Na kwa sababu wanakutana na lugha hiyo ambayo ni ngeni kwao na hawaijui, huwa inachukua muda mrefu kuwatengeneza na baadhi yao wengine wanajikuta wanaishia kukariri yale wanayofundishwa badala ya kuelewa kwa sababu ya kutokuelewa lugha ya kufundishia ya kiingereza," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa HakiElimu, John Kalage, alisema ni vema serikali ikafika mahali ifanye uamuzi juu ya lugha ipi inafaa kutumika kufundishia shuleni.

# Serikali yaipa NIMR bil. 4/- utafiti chanjo

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema imetoa Sh. bilioni nne kwa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ili kutafuta chanjo mbalimbali za magonjwa ya mlipuko.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alibainisha hayo alipofungua kongamano la kisayansi lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU).

Dk. Mollel alisema sayansi ni jicho la nchi yoyote duniani, hivyo serikali itaendelea kuwekeza kwenye sayansi ili kupata wataalamu wengi kwenye fani hiyo muhimu.

"Rais Samia Suluhu Hassan aliahidi kuipa NIMR Sh. bilioni sita kwa ajili ya kutafiti chanjo zetu wenyewe na hapa ninavyozungumza, tayari tumeshatoa Sh. bilioni nne ili watafiti waanze kazi ya kutafuta chanjo zetu wenyewe," alisema.

Naibu waziri pia alimpongeza Mwanzilishi wa Mtandao wa Elimu ya Afya Kairuki (KHEN), Hayati Profesa Hubert Kairuki kwa kuanzisha hospitali na vyuo vya afya.

Alisema uwekezaji uliofanywa na Hayati Profesa Kairuki kwenye sekta ya afya ni mkubwa na wa kuigwa kwa kuwa umesaidia kupunguza msongamano kwenye hospitali za serikali.

Alisema mtandao umekuwa na mchango mkubwa kwenye sekta ya afya kwa kuanzisha Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) ambacho kimekuwa kikitoa idadi kubwa ya wataalamu wa sekta ya afya.

"Sayansi ndiyo jicho la taifa lolote duniani, hivyo mchango wenu kwenye kuzalisha wataalamu wa afya ni mkubwa sana na serikali inathamini kazi kubwa mnayofanya, serikali itaendelea kuwasaidia na kuwaunga mkono," alisema Dk. Mollel.

Alisema serikali itaendelea kuwekeza kwenye sekta ya afya na tayari Rais Samia ameshatoa Sh. bilioni nne kwa NIMRI, ili watafute chanjo za kukabiliana na magonjwa mbalimbali.

Alisema wanasayansi lazima wajipange kukabiliana na magonjwa yatokanayo na virusi kwani dalili zinaonyesha kwamba ndilo tishio kubwa duniani kwa siku zijazo.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Profesa Yohana Mashalla, alisema magonjwa ya kuambukiza yamekuwa tatizo kubwa kwa nchi zinazoendelea kulinganisha na zile zilizoendelea.

Alisema mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 umeonyesha ni kwa namna gani taifa linapaswa kuweka mifumo imara kujiandaa kukabiliana na majanga ya aina hiyo yatakapotokea siku za mbele.

"Iko haja ya kuimarisha mifumo yetu ya afya ili tuweze kujitayarisha kukabiliana na maradhi ya mlipuko kama COVID-19 na lazima tufahamu kuwa COVID siyo ya kwanza na wala siyo ya mwisho, kuna milipuko itakuja tujiandae," alisema.





# Wakuu wa shule waonywa matumizi ya fedha za shule

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imetoa onyo kwa wakuu wa shule ambao wamekuwa wakitumia fedha za umma bila kufuata miongozo na taratibu zilizopo.

Imewaagiza wadhibiti ubora wa shule nchini kufuatilia na kusimamia uwajibikaji wa wakuu wa shule na vyuo katika kusimamia fedha miradi zinazotolewa na serikali ikiwamo za ujenzi wa shule mpya zilizopelekwa Sh. milioni 470.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Eliamani Sedoyeka, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akifunga kikao kazi cha wadhibiti hao wa kanda na wilaya kilichofanyika jijini hapa.

Alisema kumekuwapo na taarifa mbalimbali za kukosekana kwa uwajibikaji miongoni mwa wakuu wa shule.

"Mfano, serikali inatoa fedha kwa kila shule kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ila bado kuna baadhi ya shule hazitumii fedha hizo kwa wakati ili kutatua kero zinazoikabili shule kama vile uchakavu wa vyumba vya madarasa, upungufu wa madawati na vyoo bora.

"Si hivyo tu, zipo taarifa kwa baadhi ya wakuu kutumia fedha za umma bila kufuata miongozo na taratibu zinazotolewa," alionya.

Katibu Mkuu huyo aliwataka wadhibiti hao kufuata kanuni na taratibu za udhibiti ubora wa shule.

"Fuatilieni mchakato wa udhibiti ubora kwa kufanya tathmini sahihi ya nyanja za viwango vya ubora, kufanya tathmini ya ubora wa ufundishaji na ujifunzaji na upimaji mzuri na kuhakikisha kuwa walimu wanapewa msaada ya kitaalamu na kitaaluma ili kuboresha ufundishaji wao," aliagiza.

Alisisitiza kufanya tathmini ya ubora wa mtaala kujua mahitaji ya wanafunzi kwa kuhakikisha mtaala wa kitaifa unachambuliwa na kuakisi mahitaji ya mahali au muktadha.

Alisema katika kuboresha utoaji wa elimu nchini, serikali imeendelea kuboresha sekta ya elimu ikiwamo kwa kutoa elimu bila ada ili kuongeza fursa ya watoto wengi kupata elimumsingi. Kiongozi huyo alisema kikao hicho kitachangia katika kufikia mipango ya kitaifa na kimataifa kwa kuimarisha na kuboresha shughuli za udhibiti ubora wa shule kwa watendaji na wasimamizi wa elimu kuzingatia kanuni na taratibu za udhibioti ubora wa shule.

"Mnapofanya tathmini na kubaini kero zilizopo katika nyanja zote za viwango vya ubora, shirikisheni jamii kisha kuweka mkakati wa kuboresha mtaweza kuimarisha utoaji wa elimu bora na kuleta matokeo bora ya ujifunzaji," aliagiza.

Akitoa neno la shukrani kwenye kikao hicho, Mdhibiti wa Ubora wa Shule wilayani Chemba, Amon Lembao, alisema watahakikisha wanasimamia fedha za miradi zilizopelekwa kwenye maeneo yao ili ziwe na tija. Alisema watashirikisha majukwaa ya wazazi kutatua kero ya upungufu wa matundu ya vyoo na kusimamia vipindi vya dini kwenye shule ili kuondokana na tatizo la malezi kwa watoto.



Mwanamazingira ambaye pia ni Balozi wa Taifa wa mazingira mzaliwa wa mkoani Kilimanjaro, Nestory Mushi (kushoto), akipokea tuzo maalum ya taifa ya kutambua mchango wake katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira kutoka kwa Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: JAMES LANKA**

# NIT kuanza kutoa mafunzo urubani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimepanga kuanzia mwezi ujao mafunzo ya urubani yatolewe chuoni hapo baada ya kukaguliwa na mamlaka husika.

Naibu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Prosper Mgaya, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi yanayoendelea Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

"Wakufunzi wapo Afrika Kusini na hivi karibuni watafika kutoka katika mafunzo haya. Pia tumeajiri wakufunzi ambao ni wastaafu kutoka shirika la ndege ambao ndiyo tulianza nao, tumeishakaguliwa katika hatua nne za mwanzo, hapo wanakuja kuona vifaa na TCRA ni lazima wakague," alisema.

Aliishukuru serikali kwa kusaidia kuwapa mradi ambao utasaidia katika mafunzo ya usafiri wa anga na ni gharama kubwa na chuo kisingeweza.

Alisema wamejipanga kuzalisha wataalamu wengi katika nyanja za usafiri wa anga na majini kutokana na serikali kuongeza meli na ndege.

"Kwa sasa tuna mafundi na serikali tunaongeza ndege pamoja na meli tunahitaji mafundi ndiyo maana tumeanzisha kozi ya utengenezaji wa ndege, haya ni mafunzo maalum na hivyo tunawaandaa vijana wetu kufanya mitihani yenye leseni," alisema.

Pia alisema wana mafunzo kwa ajili usanifu wa meli kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu kutokana na serikali kununua na kutengeneza meli nyingi.

"Nchi yetu imezungukwa na maji na kuna boti nyingi, hivyo tumeona twende huko na tuna boti ya kisasa kule Nyasa, tunawasaidia wavuvi wadogo ili kutoa watu wenye umahiri,"alisema.

Kuhusu kozi ya madereva, Dk. Mgaya alisema wanaendesha mafunzo ya kuwajengea weledi ikiwa ni pamoja na kukabiliana na shida ya ajali ambazo zimekuwa zikitokea.

"Tumetengeneza mtaala kwa kuwatumia madereva wetu na watakuwa na umahiri katika kupunguza ajali," alisema.

# Mkakati wa kuukabili utapiamlo waanikwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema itafanya uwekezaji kitaifa wa lishe kama sehemu ya mapambano dhidi ya utapiamlo kuanzia ngazi ya kaya hadi kitaifa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati wa kikao kazi kilichohusisha watendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) na wadau wa maendeleo kuhusu masuala ya lishe nchini.

Alisema ni muhimu Taifa kuweka jitihada za pamoja katika mapambano hayo kwa kuwa ukosefu wa lishe umekuwa na madhara makubwa kwa Watanzania, hivyo kushindwa kufanya shughuli za uzalishaji kwa ufanisi.

"Uwekezaji kama Taifa katika lishe ni muhimu sana maeneo ya msingi ni elimu ya lishe ipo mikoa mingi inazalisha chakula kwa kiwango kikubwa kama Iringa na Mbeya, lakini kuna shida kubwa ya utapiamlo hasa kwa watoto na changamoto hiyo insababisha hasara kwa jamii na serikali," alisema.

Aliongeza kuwa ipo haja elimu ya lishe kufundishwa katika shule za msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba ili kuwandaa vijana kuwa mabalozi wazuri katika maeneo yao.

"Unapokosa lishe nzuri, unapata matatizo ya afya, kina mama wajawazito kukosa mtoto mwenye afya na mama mwenye afya nzuri, watoto kuwa na udumavu wa akili na mwili, Serikali itapata hasara kwa sababu ya kuwa na watu wasio na afya bora," alifafanua.

Alisisitiza ushirikishwaji wa viongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, wakuu wa wilaya na mikoa kwa kuwapatia elimu ya lishe itakayowasaidia kuwafikia wananchi katika maneo yao ili kuwa na matokeo chanya na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

"Viongozi hawa wakipatiwa elimu ya lishe bora, nini mtu ale, vyakula gani vya muhimu, maana watu wanaweza kufikiri kula chakula bora lazima uwe na uwezo, la hasha!

"Chakula kwa uwezo wowote unaweza kupangilia kikawa na tija katika mwili wako. Je, uelewa huu upo mpaka ngazi za chini? Je, nani afuatilie kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora? Lazima tutumie ngazi hizi za utawala kujenga Taifa letu," alisisitiza.

Mkurugenzi Mtendaji TFNC, Dk. Germana Leyna, alisema wataendelea kushirikiana na serikali na kuishauri, kuongoza na kumasisha lishe bpra ili kuhakikisha malengo ya nchi yanafikiwa.





Mlengwa wa mpango wa kunusuru kaya masikini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Saada Daudi Ali na mume wake, Khamis Muhammad, wa kijiji cha Makangale Pemba wakiandaa malai (ice cream) jana, ikiwa ni miongoni mwa miradi waliyoianzisha kupitia mpango huo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri: Baionuai za bahari muhimu kwa ajira Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, amesema baionuai hasa zilizo baharini na mwambao ni uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar na zimesaidia upatikanaji wa ajira kwa idadi kubwa ya watu.

Aliyasema hayo jana katika Hoteli ya Verde mjini Zanzibar wakati akifungua warsha ya nane ya kikanda kuhusu usimamizi wa mapato yanayohusiana na baionuai iliyoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP).

Waziri huyo alisema kwa kuzingatia umuhimu wake, serikali imejumuisha masuala ya baionuai katika mpango wa maendeleo ambao unalenga kuongeza maeneo ya hifadhi ya baharini pamoja na misitu ili kuhakikisha uendelevu wa mwingiliano wa kiikolojia.

Alisema sera na sheria za taasisi mbalimbali ikiwamo sekta ya mazingira na misitu zimejumuisha masuala hayo.

"Nimefurahishwa kuwa hapa kwetu tunaendelea vizuri katika utekelezaji wa programu ya Bayofin licha ya kujiunga katika hatua ya pili ni matumaini yangu kuwa tutafikia malengo na kuwa mfano bora wa upatikanaji na utumiaji mzuri wa fedha katika kuhifadhi baionuai.

Waziri huyo alisema licha ya udogo wa Zanzibar, ina utajiri mkubwa wa baionuai za majini na nchi kavu ikiwamo kima punju ambao wanapatikana Zanzibar pekee.

Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Bluu, alisema warsha hiyo inalenga kutafuta vyanzo vya mapato, msaada katika suala la uchumi endelevu na uhifadhi wa mazingira ili kusaidia nchi katika uchumi endelevu. Alisema Tanzania ina vyanzo mbalimbali ambavyo vinaweza kutumika katika uhifadhi wa mazingira na kupata maendeleo ikiwamo hifadhi ya misitu na hifadhi ya bahari.

Alisema hali ya bahari ulimwenguni sio nzuri lakini nchi mbalimbali zinachukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafunzi wa mazingira na Zanzibar bado kuna shida ya kimazingira.

Msimamizi wa Kitendo cha Mazingira kutoka UNDP, Gestrude Lyatuu, alisema wafadhili wengi wamepunguza uwekezaji katika mazingira na hata watalii waliokuwa wakichangia katika uhifadhi nao wamepungua lakini utunzaji wa mazingira ni muhimu na lazima kuendelea kuyatunza.

Alisema warsha hiyo itasaidia kuangalia vyanzo mbadala vya uwekezaji katika kuchangia kuhifadhi mazingira na kutengeneza vyanzo mbadala vya uwekezaji katika uchumi wa bluu na baionuai.

# Wanufaika TASAF waomba mikopo

**Na Rahma Suleiman, PEMBA**

WANUFAIKA wa mpango wa kunusuru kaya maskini unotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) kisiwani Pemba, wameomba kupatiwa mikopo itakayoimarisha miradi ya kiuchumi waliyoianzisha.

Walisema jana kuwa miradi mingi waliyoianzisha kutokana na ruzuku wanazopokea kupitia mpango huo, inahitaji mwendelezo ili kufikia azma ya serikali ya kuondoa umaskini na kuzifikia ndoto zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari wa habari waliokuwa katika ziara ya maofisa wa TASAF waliotembelea wanufaika wa Kijiji cha Makangale, Mkoa wa Kaskazini Pemba, waliishukuru TASAF kwa kuwapatia mtaji wa biashara na shughuli za kiuchumi zilizobadilisha maisha yao.

"Kabla ya kuingia kwenye mpango huu, hali ya maisha ilikuwa ngumu kiasi ya kwamba hatukumudu milo miwili, jambo ambalo sasa kwetu ni historia," alisema Saada Daudi Ali, mkaazi wa kijiji hicho (36) anayenufaika na mpango huo.

Sada ambaye ni mama wa watoto sita anayejihusisha na biashara ya nguo, juisi na icecream, alisema iwapo atapata mkopo, anakusudia kufungua duka na kununua vitendea kazi vya kisasa vitakavyokuza biashara hizo.

Aliipongeza serikali kwa kuanzisha mpango huo ambao umefungua fursa za kujiendeleza kiuchumi na kupunguza umaskini wa kaya zao.

Mume wa mnufaika huyo, Khamis Hamad, alipongeza hatua ya serikali kuwawezesha kiuchumi wananchi na kuwaomba wanufaika wengine kutumia vizuri fedha wanazopatiwa.

"Ingawa fedha tunayopata ni ndogo lakini kama utajiongeza na kuzitumia vizuri, fedha hizi zinaweza kutumika kuibua miradi ambayo inapunguza unyonge na umaskini," alisema.

Mtumwa Fadhil Hamad alisema ruzuku anayopatiwa anaigawa kwa ajili ya matumizi ya watoto shuleni na kiasi kidogo anakiwekeza kupata ujuzi wa uchoraji na kusuka mikoba, makawa na vifaa vingine vya ukili.

"Kwa kweli nimepata manufaa makubwa na kazi ninayoifanya sasa inatokana na fedha za TASAF ila kama nitapata uwezeshaji zaidi, ninaamini nitamudu kununua vifaa vya kisasa na kuhimili gharama za malighafi," alisema Mtumwa.

Alisema kuwa hatua hiyo itachochea ukuaji wa uchumi wa kaya yake na kupunguza umaskini wa kipato unaowakabili ikiwa ni pamoja na kumudu kasi ya ushindani katika soko kwa kuzalisha bidhaa bora zaidi.

Katika ziara hiyo, maofisa hao walitembelea miradi mbalimbali ya walengwa wa mpango huo inayohusisha biashara na upandaji wa miti kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira kuzunguka eneo la Hifadhi ya Taifa ya Msitu wa Ngezi uliopo katika Shehia ya Makangale kisiwani Pemba.

## Serikali kuyapa kipaumbele magonjwa yasiyoambukiza

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema imejipanga kuhakikisha maradhi yasiyoambukiza yanapewa kipaumbele kwa kuongeza vituo vya afya kwa ajili ya kuchunguza afya zao mapema.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidha, alibainisha hayo jana alipojibu swali la Mwakilishi wa Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua mikakati ya wizara katika kupambana na maradhi yasiyoambukiza nchini.

Khamis alisema maradhi yasiyoambukiza ambayo ni pamoja na kisukari, shinikizo la damu pamoja na saratani ni tishio kwa afya za wananchi ambayo yanatibika kama wananchi watachunguzwa afya zao mapema.

Alisema vituo vya kuchunguza afya za wananchi katika maradhi yasiyoambukiza vimeongezeka na kufikia 55 hatua ambayo imetoa fursa kubwa kwa wananchi kuvifikia.

Naibu waziri huyo alisema tayari jumla ya watu 4,951 wamechunguzwa afya zao na kupimwa ugonjwa wa kisukari wakati wananchi 16,192 walipima afya zao kwa ajili ya ugonjwa wa shinikizo la damu.

"Mheshimiwa Spika, tumeanza kupima wananchi wetu magonjwa yasiyoambukiza ambayo ni kisukari, shinikizo la damu pamoja na saratani ili kukabiliana na magonjwa hayo katika hatua za awali," alisema.

Alibainisha kuwa kwa ugonjwa saratani, jamii imekuwa ikihamasishwa kujitokeza kupima ugonjwa huo ambapo waanafunzi wa shule za msingi na sekondari wamepewa kipaumbele.

Alisema jumla ya wanawake 12,212 wamechunguzwa afya zao kubaini kama wana saratani ya shingo ya kizazi ambapo wanawake 371 walibainika na maradhi hayo na kuanza kupatiwa katika hatua mbalimbali.

ZUCHU
UKURASA 13



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI JUNI 11, 2022



# ROSE MHANDO TENA
## Ya nyuma yaishe, sasa kurina asali

MALKIA wa muziki wa Injili nchini, Rose Muhando, ameanza kunyanyuka tena baada ya kupotea kwa miaka mingi, huku akipita katika mazingira magumu ambayo kuna wakati yalimkatisha tamaa.

Hata hivyo, mwimbaji huyo ambaye alikuwa maarufu Afrika Mashariki kutokana na nyimbo zake nzuri za Injili, ameamua kurudi tena jukwaani na kutoa nyimbo mfululizo ambazo zimeanza kumrudisha tena jukwaani.

Wimbo wake mpya 'Tuipakue Asali' ameutambulisha mapema wiki hii, akisema ni sawa na mwanga unaomwangazia kuona njia sahihi.

Rose, ameliambia BT, kwamba wimbo huo unatokana na ile safari ndefu ya wana wa Israel kutoka Misri kwenye nchi ya ahadi yenye asali na maziwa na kupitia changamoto nyingi kabla ya kupata ushindi.

"Ni wimbo wa kufurahia ushindi na kuipakua asali na maziwa kwenye nchi ya Kaanani tuliyopewa na Mungu, huko hakuna shida ni kufurahia ushindi," amesema Rose.

Amesema sasa anaangalia mbele katika safari yake ya muziki na kamwe hawezi kurudi nyuma.

BASI SAWA

## Phantom Musica wataja 'Donda la Moyo' balaa



KUNDI la muziki wa dansi la Phantom Musica International la jijini Dar es Salaam linazidi kutetemesha mashabiki baada ya kuibuka na kibao kipya kinachojulikana 'Donda la Moyo'.

Abdulfareed Hussein ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kundi hilo, amesema wimbo huo umebeba maudhui ya maisha ya kila siku ya ndani ya jamii.

Amesema, kukamilika kwa wimbo ni unalifanya kundi hilo kuwa na jumla ya nyimbo sita hadi sasa ambazo tayari zimekamilika.

Akiuzungumzia wimbo 'Donda la Moyo', Mkurugenzi huyo alisema ni kazi nyingine inakwenda kuliweka juu kundi hilo kwasababu imewashirikisha baadhi ya wanamuziki wazoefu.

Aliwataja kuwa ni King Budas, Edo Sanga na Zagredo Butamu ambapo katika safu ya wapiga ala wameshiriki Fadhili Musafi, Chimuz Chinyama na na Ababa Fayeed.

## Joh Makini ashtuki na kiki zenu



RAPA mkali Joh Makini, amesema wasanii wa bongo hawana kiki ambazo zinaweza kumstua au kumshangaza.

Amesema baadhi ya wasanii wanaofanya mambo hayo hawajui nini wanachokifanya kutokana na mipango yao kusikika kabla ya kutoa hadharani.

"Hakuna drama wala kiki yoyote ambayo imewahi kufanywa na wasanii wa Bongo ikawahi kunishtua au ikanifanya nikaiamini, wanajua ni kwa sababu gani wanafanya hata watu wengine unakutana nao wakati wanapanga hiyo mipango kabla ya kwenda Public" amesema.



## WAJIULIZE WALIPOTELEZA

SASA ni wazi wanamuziki wanaotamba katika ukanda wa Afrika Mashariki, wanatakiwa kujiuliza wapi wameteleza, baada ya kuangukia pua katika tuzo za BET 2022.

Wanamuziki kama Diamond Platnumz, Harmonize, Ali Kiba na Sauti Soul, majina yao hayakuchomoza katika kuwania tuzo hizo, badala yake wasanii kutoka Nigeria, DRC na Afrika Kusini wanatamba.

Tuzo hizo zinatarajiwa kutolewa Juni 26 huko Los Angeles nchini Marekani.

Hata hivyo, kipengele ambacho kinawabeba wanamuziki wa Afrika ni kile cha Best International ACT, ambacho hakuna hata jina moja la msanii kutoka Afrika Mashariki.

Kipengele hicho kina majina kama Dave (Uingereza), Dinos (Ufaransa), Fally Ipupa(DRC), Fireboy DML (Nigeria), Littler Simz (Uingereza), Ludmilla (Brazil), Major LeagueDj'z (Afrika Kusini), Tayc (Ufaransa na Tems (Nigeria).

Kutokana na hali hiyo, ni muhimu kwa wasanii wa muziki nchini kuanza kutafuta wapi wamekosea na kushindwa kupenya katika orodha hiyo, badala ya kuendeleza majigambo na chuki dhidi yao wenyewe.

# Kunguni: Umbeya si kazi, tatizo kusutwa

Na Adam Fungamwango

EEEH mwaya, umbea siyo kazi, kazi pale uliokuwa unawafanyia hivyo wakigundua kuwa wewe ni mnafiki, mgombanishi na muongo, ndiyo utakapojua kuwa hujui.

'Kunguni' ni filamu inayoonyesha maisha ya baadhi ya watu uswahilini, maarufu kama 'uswazi'. Uswazi bwana kuna mambo.

Kuna watu wanagombana, wanaachana, hata wakati mwingine kushtakiana kwa vitu vya uongo. Kwa vitu ambavyo kuna mtu amekaa huko na kuvitengeneza na kuvisambaza kwa lengo ya ugombanishi.

Wengine wanawaita vizabizabina, au pangukavu tua mchuzi.

Filamu imechezwa na Salim Ketemo, Careen Kitajo, Rayuu Chande, Dorah Martin na wengineo.

Kwenye eneo moja huko uswazi kuna dada mmoja anaitwa Hadija Nyolo. Huyu ni mbea balaa.

Huyu akiamka anakusanya data za watu, huyu kala nini, anaishi vipi, anatembea na nani, kila habari ya familia anaijua yeye, lakini yote hayo alikuwa anaundaunda habari, ni mzushi, mchonganishi.

Na mwenyewe anajisifu akidai ni mtetezi wa wanyonge, amezaliwa kwa kazi maalum ya kusaidia wanaotetwa.

Hadija anawakuta Careen na mpenzi wake Kumoso wamekaa sehemu wakaongea mambo yao ya mapenzi.

Yeye akaenda kwa shoga yake mkubwa kiasi cha kuitana dada, mke wa Mbinde na kumweleza kuwa amewasikia wapenzi hao wakiwateta yeye na mumewe.

Yaani yeye mke ni mchafu na hajui kuoga, hajui mapenzi na pia mumewe anafanya kazi ya kuokota chupa tu mitaani.

Umbea huo siyo tu umewafanya mke wa Mbinde na Careen wagombane, lakini ulileta mzozo kati ya Mbinde mwenyewe na mkewe, wakituhumiana kutoa siri zao.

Siyo hao tu, akaanza kufarakanisha ndoa za watu, pamoja na urafiki wa wanawake wenzake.

Mwanamke mmoja akaamua kutengeneza mbinu kwa sababu ni yeye pekee aliyegundua Hadija ni muongo.

Akampa simu Carren kwenda kumuuliza maswali kama mwandishi au mpelelezi. Kazi ya hiyo simu ni kumrekodi.

Careen alimuuliza maswali kiujanja Hadija, na yeye akawa anafunguka bila kujijua kama anarekodiwa.

Akatapika yote kuwa anasema huwa si ya ukweli, lakini yake yeye ni kufitinisha tu, na hata yeye amemfitinisha kwa sababu urafiki wake na mke wa Mbinde unamkera sana kwani ni kama undugu.

Majirani wote sasa wakajua kumbe 'mchawi' wao ni Hadija ndiye anayewagombanisha. Wanawake wa mtaa wakafungia kazi, na kumuelenda nyumbani kwake na 'kigoma cha Uruguay' matarumbeta juu, kwenda kumsuta.





## Zuchu azidi kuwasha taa nyekundu

MWANAMUZIKI nyota wa kike wa BongoFleva, Zuchu, amevunja rekodi katika ukanda wa Afrika Mashariki, baada ya kuwa na wafuasi zaidi ya milioni 2 wanaoweza kuona kazi zake katika mtandao wa You Tube.

Zuchu aimefikisha idadi hiyo ya watu wanaoweza kuona moja kwa moja kazi zake 'Subscribers' Milioni 2 ndani ya miaka miwili pekee.

Kutokana na takwimu hito, sasa Zuchu anakuwa msanii wa nne wa kike Afrika, wenye wafuasi wengi wanaoweza kumfuatilia mtandaoni.

## BENDI 5 KALI ZA MASHIRIKA YA UMMA

Na Adam Fungamwango

BAADA ya Azimio la Arusha mwaka 1967, zilianzishwa bendi nyingi za mashirika ya umma nchini Tanzania.

Lengo ni kutoa burudani kwa wananchi, kuelimisha, kuhamasisha wananchi kunapokuwa na hafla mbalimbali za kiserikali na kichama, lakini ilikuwa ni sehemu ya kuingiza kipato kwenye mashirika hayo.

Si kwenye mashirika hayo tu, bali kwenye Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jumuiya za Chama kukawa na bendi ya Juwata Jazz 'Msondo Ngoma', iliyokuwa ikimilikiwa na Jumuiya ya Wafanyakazi ya Tanzania, Vijana Jaz, iliyokuwa chini ya Jumuiya ya Umoja wa Vijana Tanzania na hata bendi za watu binafsi.

Leo tunaziangazia bendi zilizokuwa zinamilikiwa na mashirika ya umma Tanzania.

**Biashara Jazz Band**

Ni bendi ilioanzishwa mwaka 1975, ikimilikiwa na Shirika la 'Stade Trade Corporation', ambalo lilikuwa likifanya biashara za ndani ya nchi. Bendi hiyo ikaitwa kwa kifupi STC Jazz. Ndiyo bendi ya kwanza kabisa ya Marijani Rajab, kabla hajahamia Safari Trippers na baadaye Dar International.

Baadaye shirika hilo likabadiliwa na kuwa Bodi ya Biashara ya Ndani 'Board of Internal Trade', hivyo kuifanya bendi hiyo kubadilisha jina na kuwa Biashara Jazz Band.

Ilipobadilisha jina na kuitwa Biashara Jazz, Marijani alikuwa ameondoka, kiongozi wa bendi hiyo akawa Juma Ubao 'King Makusa' na ilirekodi nyimbo mbalimbali, zilizokuwa maarufu sana ni 'Posa Nitaleta', 'Kipini cha Dhahabu' na nyinginezo.

**UDA Jazz Band**

Ilimilikiwa na Shirika la Usafiri Dar es Salaam. Ni kama vile kwa sasa UDAT imiliki bendi ya muziki wa dansi. Ilianzishwa miaka ya 1980, baadhi ya waanzilishi ni Benovilla Antony, Hamza Kalala na hata TX Moshi William alikuwamo kwenye kuanzisha bendi, lakini kabla haijaanza kurekodi alirejea kwao Tanga, na hata aliporejea Dar alijiunga na Polisi Jazz ndipo umaarufu wake ulipoanza, kabla ya kuchukuliwa na Juwata Jazz Band.

Ina nyimbo nyingi maarufu kama 'Tulele Tuboe', 'Nenda Kaishi Salama', 'Uteti', 'Sakina', "Nachunga Heshima' na nyinginezo.

**Urafiki Jazz Band**

Kiwanda cha Nguo Urafiki maeneo ya Ubungo, Dar es Salaam kilimiliki bendi walioiita Urafiki Jazz. Ilianzishwa mwanzoni mwa mwaka 1970.

Juma Mrisho 'Ngulimba wa Ngulimba' ndiye aliyekuwa kiongozi wa bendi hiyo. Ilikuwa na nyimbo mbalimbali maarufu kama 'Paulina', 'Gezaulole', 'Rukia', 'Kwa Mjomba', 'Rudisha Pete Lucy' na nyingine nyinginezo.

**Bime Lee**

Bendi hii ilimilikiwa na Shirika la Bima la Taifa. Ilianza miaka ya 1970, na ilipitia kwenye awamu mbalimbali na wanamuziki mbalimbali maarufu kama kina Joseph Mulenga, Jumbe Batamwanya, Roy Bashekanako, Athumani Momba, Shaaban Dede, Selemani Mwanyiro, Abdallah Gama, Jerry Nashon 'Dudumizi' na wengine wengi.

Mtindo wao maarufu ulikuwa ni 'Magnet Tingisha'. Nyimbo zao maarufu ni 'Makulata', 'Neema', 'Asia', 'Pesa Zaniisumbua','Shangwe na Harusi', 'Sophi' na nyingine nyingi.

**Washirika Tanzania Stars**

Ilianzishwa rasmi Agosti 1989 ikiwa inarithi jina la bendi ya Tanzania Stars ambayo ilikuwa chini ya Vyama vya Msingi vya Ushirika ikiwa inafanya maonyesho yake kwenye Hoteli ya Maggot pale Mtaa wa Samora jijini Dar es Salaam. Bendi hiyo ilibadili jina mara tu ilipoanza kumilikiwa na Muungano wa Vyama vya Ushirika Tanzania na kuitwa Washirika Tanzania Stars na kuwachukua wanamuziki kamaAdam Bakari, Eddy Sheggy, na Hamza Kalala.

Nyimbo zao ni kama 'Penzi la Ulaghai', 'Shakaza', 'Nimekusamehe', 'Jully', 'Watoto Wamekuja juu' na nyinginezo.



## Wizkid, Tiwa wana jambo zito

WASANII nyota wa muziki nchini Nigeria, Wizkid na Tiwa Savage, wameibua minong'ono baada ya kuonekana pamoja wakila bata nchini Marekani.

Ni mara yao ya kwanza kwa wasanii hao kuwa pamoja kwa muda mrefu wakifanya matanuzi, jambo ambalo limezidisha joto kwa mashabiki wao kwa kuhisi kuna jambo zaidi katika urafiki wao.

Kila mmoja aliamua kwenda Marekani katika jiji la Los Angeles kwa ajili ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa mara baada ya kufanya matamasha yao ya muziki. Hata hivyo swali limebaki kuwa wasanii hao kuna zaidi ya hapo?



## Alex waeleze vizuri, pengine watasikia

ALIYEKUWA mshiriki wa shindano la Big Brother Naija, Alex amesema wanawake wanaobadilisha maumbo yao kwa upasuaji wanajiweka katika hatari kubwa ya kiafya.

Akishiriki katika mtandao wa Snapchat, amesema wale ambao wanataka kufanya hivyo, kwanza wamtazame mama zao ambao miaka yote wanafurahia maumbile yao halisi.

"Maoni yangu kama huna tatizo la kiafya, lakini unataka kubadilisha mwili kutokana na urembo utakuwa hauko sawa ni lazima uguse sura yako na ujiulize zaidi," amesema.


## Burna Boy sasa umezidi

MKALI wa muziki kutoka Nigeria, Burna Boy, inaelezwa kwa sasa amekufa katika mapenzi mazito na mshiriki wa Big Brother Naija, anayeitwa Nengi.

Wote wawili wameonekana katika klabu moja ya usiku wakiwa wameshikana mikono muda wote.

Nengi alionekana kila mara akimfuta jasho  Burna Boy, kwa kutumia kitambaa chake huku akimshika kiunoni.





## We Kim unachokisema kinatoka moyoni?

MWANAMITINDO maarufu nchini Marekani, Kim Kardashian, amezua gumzo baada ya kusema kuwa yupo tayari kula hata kinyesi ilimradi aendelee kuonekana kuwa bado mdogo.

Wakati anafanyiwa mahojiano na kituo cha New York Times, mama watoto huyo wa Kanye West, amesema kuwa anaweza kufanya hivyo hata kila siku kama kitakuwa na faida kwake.

"Kama ungeniambia kuwa natakiwa nile kinyesi kila siku na nitaonekana bado mdogo ningefanya hivyo," amesema na kumshangaza mtangazaji.

## Depp ambwaga mkewe kortini

MTAYARISHAJI wa filamu kutoka Marekani, Johnny Depp ameshinda kesi ya kashfa ya unyanyasaji dhidi ya mke wake wa zamani Amber Heard.

Depp, ambaye hakuwa kortini wakati wa hukumu, alishtaki na kudai dola milioni 50 kama fidia kutokana na chapisho la mwaka 2018 , kupitia gazeti la The Washington Post, akidai alikashfiwa.

Mahakama iligundua kwa pamoja kwamba Heard hakuweza kuthibitisha madai yake dhidi ya Depp na kwamba alijua madai yake ya unyanyasaji yalikuwa ya uwongo alipochapisha kupitia chapisho lake hilo mwaka 2018.



MAKALA

# HIZI NDIZO FAIDA KIKOKOTOO KIPYA

## ■ Wastaafu kumwagiwa fedha miaka yote
## ■ Hakuna atakayeishi kifukara kama nyuma

Na Sabato Kasika



SERIKALI kupitia Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, imetangaza kukamilika kwa maandalizi ya kanuni mpya ya ulipaji wa pensheni kwa wastaafu.

Katika taarifa yake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Jamal Katundu, ametoa ufafanuzi kuhusu ulipaji wa mafao maarufu kama kikokotoo akiwa jijini Dodoma.

Prof. Katundu anasema, kikokotoo kipya kitaanza kutumia kuanzia Julai Mosi, mwaka huu na kwamba kitawanufaisha wastaafu.

Kuanzishwa kwa kikokotoo hicho kipya cha asilimia 33, badala ya 25, ni baada ya Rais Samia Suluhu kutangaza kuridhia ongezeko hilo.

"Namshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia maombi ya wadau wa sekta ya hifadhi ya jamii yakihusisha, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) kwa kukubali kupandisha asilimia ya kikokotoo," anasema Prof. Katundu.

Prof. Katundu anasema kanuni mpya inaongeza kiwango cha malipo ya mkupuo kutoka asilimia 25 iliyokataliwa mwaka 2018, hadi asilimia 33 kwa wanachama wote 1,364,050.

"Asilimia 81 ya wanachama wote wa mifuko ya pensheni mikupuo yao inaongezeka kutoka asilimia 25 hadi asilimia 33," anasema na kuongeza: "Hii ina maana kuwa, Serikali ya Rais Samia imesikia kilio cha wastaafu na kuridhia malipo ya mkupuo kwa kuwajali Watanzania hawa."

Kwa nyakati tofauti, Nyanda na Katibu Mkuu Katundu wanabainisha kuwa, wanachama wote wa mifuko watanufaika na ongezeko hilo kwa kupanda asilimia 81 ya wanachama wa mifuko hiyo ambao ni wengi zaidi.

Awali wanachama wa mifuko mingine ambao awali walikuwa wanapata mkupuo wa asilimia 50.

"Kanuni inaongeza pensheni ya mwezi kutoka asilimia 50 ya sasa hadi asilimia 67 kwa waliokuwa wanachama wa PSPF na LAPF ambao ni asilimia 19 ya wanachama wote wa mifuko ya pensheni. Hapa utaona kila mstaafu sasa ananufaika," anaongeza Prof. Katundu.

Kwa upande wa Nyanda anafafanua kwamba watu wengi huwa hawaelewi ukweli kwamba, kadiri unavyochukua kiasi kikubwa kwa mkupuo mmoja, ndivyo utakavyopata pensheni ndogo ya kila mwezi na kusababisha ugumu katika maisha yako ya kustaafu.

Nyanda anasema ndio maana hata hao asilimia 19, wanapata manufaa makubwa kwa kuwa pensheni yao ya kila mwezi itakuwa kubwa kuliko ilivyokuwa awali.

Faida nyingine kwa mujibu wa Profesa Katundu, ni kwamba, kikokotoo kipya mifuko ya pensheni ya PSSSF na NSSF itaimarika na kuwa endelevu na mifuko inaweza kuongeza pensheni ya kila mwezi kwa kuzingatia tathmini zitakazofanyika kila baada ya miaka mitatu hivyo, wastaafu kuendana na hali halisi ya maisha.

Kamishna huyo wa Tume ya Haki za Binadamu, Nyanda Shuli, anasema hifadhi ya jamii huimarisha ustawi wa watu kwa kuweka mifumo ya kukinga wananchi dhidi ya majanga ya kijamii kama uzee, ulemavu, kifo, ugonjwa na kukosa ajira.

"Ipo mifumo ya uchangiaji na isiyo ya uchangiaji (misaada). Mifumo ya uchangiaji ina wanachama wanaochangia na hivyo kustahili huduma kulingana na sheria na kanuni zinazotumika," anasisitiza Shuli.

Anasema, mifumo ya uchangiaji huipunguzia serikali mzigo kupitia bajeti yake huku ile isiyo ya uchangiaji ikiwa ni misaada kama vile Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na huduma za afya kwa wazee na makundi mengine.

Anasema, vyanzo mbalimbali vinabainisha kuwa, kabla ya Uhuru ilikuwapo mifuko ya GEPF (1942) na LAPF (1944) na baada ya Uhuru yaani mwaka 1962, serikali ilipanua wigo kwa watumishi wa serikali kujumuisha walimu.

"Mwaka 1964 ulianzishwa Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa Umma na wa Sekta Binafsi (NPF na baadaye NSSF) na mwaka 1978, ukaanzishwa Mfuko wa Pensheni - Watumishi wa Mashirika ya Umma (PPF) na hatimaye mwaka 1999, Serikali ilikabadilisha mfumo wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali Kuu uliorithiwa wakati wa Uhuru na kuwa katika mfumo wa uchangiaji na kuanzisha mfuko wa PSPF," anafafanua zaidi.

Anasema, mwaka 2018 ilitungwa Sheria Na. 2 ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) iliyounganisha Mifuko ya GEPF, LAPF, PPF na PSPF na kuwa mfuko mmoja; na hapo, ikaanzishwa kanuni ya mafao ya pensheni ambayo kimsingi, ilikataliwa na wadau.

Anafafanua kuwa, Mkurugenzi wa Hifadhi ya Jamii, Festo Fute, alisema kuunganisha mifuko hiyo mwaka 2018 kwa PSSSF kulilenga hasa kuokoa mfuko wa PSPF usife, kupunguza gharama za uendeshaji, kuifanya mifuko kuwa endelevu, kuweka uwiano wa mafao kwa wastaafu wote, kuongeza ufanisi wa huduma na kuondoa ushindani usiokuwa na tija kwa umma.

Vyanzo vinataja sababu za kukataliwa kwa Kanuni ya Kulipa Mafao ya Pensheni 2018 kuwa zilikuwa ni pamoja na kupungua kwa kiwango cha malipo ya mkupuo, wadau kutokukubaliana kuwapo malalamiko.

**MAELEKEZO YA SERIKALI**

Anasema kutokana na hali hiyo, Desemba 28, 2018 serikali ilitoa maelekezo ya kusitisha utekelezaji wa kanuni iliyopendekezwa na pia, wadau yaani serikali, waajiri na wafanyakazi wakatakiwa kukaa na kukubaliana kanuni itakayokubaliwa na pande zote na kanuni za awali ziendelee kutumika katika kipindi cha mpito kutoka mwaka 2018 hadi 2023.

kwamba ili kutekeleza maelekezo ya Serikali na kuwa na uamuzi sahihi, aliajiriwa mtaalamu elekezi kutathmini uendelevu Mifuko ya PSSSF na NSSF na ikaundwa pia kamati ya wataalamu kuchambua taarifa ya mtaalamu elekezi ili kuishauri kamati elekezi na pia, kufanya utafiti ili kupata uzoefu kutoka nchi nyingine.

Anasema matokeo ya uchambuzi wa mifuko kwa PSSSF yalibainisha kuwa, kikokotoo kinachotumika hakina uwiano na michango ya asilimia 20 na kwamba, ifikapo mwaka 2034, mfuko utashindwa kulipa mafao kwa wastaafu.

Ikabainika kuwa, ili kuendelea kulipa mafao kama ilivyo sasa, michango ya wanachama na mwajiri inabidi iongezeke kutoka asilimia 20 ya sasa mpaka asilimia 25.70. Hili, lingeongeza machungu kwa waajiriwa maana lingepunguza mshahara waupokeao mkononi na kuongeza makato.

"Sehemu kubwa ya fedha inatumika kulipa malipo ya mafao ya kukosa ajira ambayo si lengo kuu la mfuko, NSSF ingeshindwa kulipa mafao kwa kutumia kiwango cha sasa cha michango ifikapo mwaka 2042," anasema.

Kwa mujibu wa Nyanda, ili kuendelea kulipa mafao kama ilivyo sasa, michango ya wanachama na mwajiri inabidi iongezeke kutoka asilimia 20 ya sasa mpaka asilimia 23.20, na kwamba ingeongeza machungu kwa waajiriwa.

"Hivyo, kanuni iliyokubaliwa katika machakato huo ulioshirikisha wafanyaklazi kupitia vyama vyao, waajiri na serikali, inatoa kiwango cha mkupuo cha asilimia 33 badala ya asilimia 25 na itazingatia kipindi cha ajira; na kikokotoo limbikizi ni 1/580," anasema.

Anaongeza kuwa lililokubaliwa na wadau wote ni makadirio ya wastani wa miaka 12 na nusu baada ya kustaafu pamoja na kutumia wastani wa mishahara ya miaka mitatu ndani ya miaka kumi kabla ya kustaafu katika kukokotoa mafao ya pensheni ya mstaafu.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOKWENDA...

# Kutoka kunyoa chini ya mwembe hadi saluni



Na Adam Fungamwango



Hii ndiyo ofisi ya vinyozi wa zamani, hapo kinyozi akinyoa nywele mteja chini ya mti, kwani enzi hizo hakukuwa na saluni kama hivi sasa.

KWELI waswahili wanasema kila kitabu na zama zake. Miaka ya sasa ukitaka kunyoa unatoka nyumbani kwako kama na gari, bodaboda au hata kwa miguu na kwenda saluni kunyoa nywele.


Kwanza kabisa unakutana na fremu moja lililopo kwenye jengo zuri, iliyonakshiwa maandishi yenye urembo, bila kusahau neno saluni ukiliangalia kwa juu.

Unafungua mlango na kukutana na hali ya hewa tofauti na ulikotoka. Ni baridi kali ya bandia lililotengezwa na kirekebisha hewa kilichopo ndani.

Unakaribishwa kwenye kiti ambacho mpaka upande kidogo juu, miguu ining'inie. Anayekukaribisha ni kijana asiyepungua miaka 20 na asiyezidi miaka 27. Pande zote nne zimezungukwa vioo, ukijitazama mwili mzima kuazia juu mpaka viatu ulivyovaa. Wakati mwingine kunakuwa na sehemu moja ya vioo na nyingine picha mbalimbali za watu na wasanii wakubwa duniani, wakiwa wamenyoa mitindo mbalimbali ya nywele. Kama ni saluni isiyo na kipoza hewa, basi utakuta juu na pembeni zimefungwa feni, huku chumba kizima kikizungushiwa vimbwanga kibao.

Wakati mnyoaji ukiwa umepanda juu ya kiti, pembeni na chini ya kuta kuna makochi manene mazuri yenye nakshi za kila aina.

Kijana aliyekukaribisha anakuvalisha kitambaa kikubwa kuzuia nywele kuganda kwenye nguo, na kuanza kukunyoa kwa staili unayotaka. Ananyoa kwa mashine. Anatumia pia kitana. Anaponyoa kuna wakati anakupaka poda, kwa sababu mbalimbali zinazohusiana na kazi yake.



Kijana akinyolewa nywele na mwenzake nyumbani enzi hizo, kama hutonyolewa chini ya mti basi itakuwa ni nyumbani na kwenye mazingira kama haya.

Akimaliza anakufuta poda na nywele kwa kutumia taulo, baadaye anakupaka dawa yenye harufu kali, ambayo kazi yake ni kuua vijidudu ambavyo vinaweza kuwemo na kusababisha magonjwa ya ngozi.

Ghafla anakuja dada mmoja mrembo na kukuuliza "mzee tukuoshe na uso?' Au "Mzee tukufanyie masaji ya uso?"

Hapa sasa hafundishwi mtu, ni hiyari yako, kukataa au kukubali na wala hulazimishwi.

Kama ukikubali utaingizwa chumba kidogo pembeni na kuoshwa uso na maji safi ya uvuguvugu, wakati huohuo utaulizwa kama atumie losheni kupaka usoni.

Inawezekana kabisa mrembo huyo baadaye akakuuliza tena "mzee tuoshe miguu?" Yote hayo nimesema kukubali au kukataa ni hiari yako.

Yote haya yanayofanyika sasa ni tofauti kabisa na zamani. Kila kitu kimebadilika. Ukikumbuka jinsi watu walivyokuwa wakinyoa zamani na sehemu zenyewe za kunyoa unabakia unacheka kimoyomoyo tu.

Na ukimhadithia kijana wa leo, wengine wanaweza wasiamini na wengine, wakabaki midomo wazi.

Enzi zile mtoto, kijana au mzee kunyoa ilikuwa ni lazima unyolewe na mwanaume mwenzako. Labda kama mtoto mdogo wa kike ndiye anaweza kunyolewa na mwanaume.

Msichana au mama mzima ni lazima anyolewe na mwanamke mwenzake.

Wakati ule vinyozi walikuwa wa aina kuu mbili. Walikuwepo ambao walikuwa wamekodisha vyumba, siku hizi wanaita fremu na utakuta kibao nje kimeandikwa 'kinyozi anapatikana hapa.' Hao walikuwa wachache sana na inawezekana waliokuwa wananyoa sehemu kama hizo ni watu maarufu na wenye nyadhifa kubwa serikalini.

Wengine walifanya kazi zao chini ya miti. Hao sasa ndiyo wengi sana, na kizazi kingi cha wakati huo ndiyo kilikuwa kinanyoa sehemu kama hizo.

Yoyote aliyezaliwa miaka ya 1990 kurudi nyuma, atakwambia alishawahi kunyoa chini ya mti.

Mara nyingi miti yenyewe ni mwembe, mkungu, au mti wowote ule mkubwa hivi.

Picha linaanza ukifika tu hapo unakutana na kinyozi ambaye ni mtu mzima sana. Tofauti na vinyozi wa sasa ambao ni vijana sana.

Ofisi yake ina kioo kikubwa ambacho amekiegemeza kwenye mti, halafu ana mkoba wake pembeni wenye mikasi, wembe, vitana na chanuo.

Ukifika hapo unakaribishwa kwenye kiti cha malimba, au kilichotengenezwa kwa mbao, halafu unafungwa kitambaa kikubwa cheusi ambacho ni kaniki, au cheupe, wakati mwingine chenye rangi ya bluu.

Baada ya hapo unaanza kunyolewa staili unayotaka mwenyewe kama unanyoa ndevu sawa, kipara, denge au staili mbalimbali za kisasa wakati huo ikiwemo ile ya Oscar Kambona. Wenyewe watu wa enzi hizo wanaujua. Kila mnyoo na bei yake.

Hata watoto wadogo, siku za kukaribia kufungua shule, wanasafiri au karibuni na sikukuu, hupelekwa kwa vinyozi hao wa chini ya mti.

Watoto hasa wa kiume hunyolewa nyumbani siku za kawaida tu, kwenye mpango mkakati wa kupunguza urefu wa nywele zake, lakini kama anatakiwa apendeze, atapelekwa 'kwa kinyozi'.

Sasa ukute ndiyo kipindi au msimu wa wale wadudu ambao wanaitwa washawasha au 'chavichavi' ni balaa tupu.

Kuna wale wadogo ambao huwa hawaonekani vizuri, lakini wakikutambaa wanawasha sana na hata nguo uliyovaa kama ameingia ukiivaa inakuwa hivyo hivyo, mwenyewe utaivua.

Halafu kuna wale ambao ni wakubwa. Sasa wakati uko kwa kinyozi wanaweza kukuangukia, hivyo ni lazima uwe tayari kwa hilo.

Pale kwa kinyozi chini ya mti pembeni mara nyingi huwa na mabenchi ya magogo, tofauti na makochi ya ndani ya saluni. Hapo utawakuta wazee na watu wengine wakiwa wanapiga mastori ya hapa na pale.

Habari zote za kijamii, kisiasa, utamaduni, udaku na hata michezo utazikuta hapo.

Halafu hatua kadhaa tu unaweza kukuta kuna muuza kahawa nae anafanya biashara yake, hivyo sehemu hiyo kuifanya kuchangamka na kufikiwa na watu wengi.

Kwa uchache tu hii ndiyo tofauti na vinyozi wa zamani, pamoja na mandhari ya maeneo husika.

**Tuma meseji 0716 350534**



Mteja akinyolewa kwenye saluni ya kisasa yenye kila aina ya vifaa, vikorombwezo na nakshi nyingi.

# Putin ajigamba Ulaya haitaweza kususia nishati ya Russia kwa miaka mingi

**MOSCOW,** RUSSIA

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amesema nchi za Magharibi hazitaweza kususia mafuta na gesi kwa miaka kadhaa.

Kiongozi huyo aliongeza kuwa hakuna mtu anayejua nini kinaweza kutokea wakati huo, kwa hivyo kampuni za nchi yake hazitatengeneza visima vyao vya mafuta.

Kauli hiyo inakuja siku chache baada ya ofisa wa Marekani kukiri kwamba Russia inaweza kupata faida zaidi kutokana na nishati hizo kuliko ilivyokuwa kabla ya vita.

Muungano wa Ulaya( EU) inaagiza karibu asilimia 40 ya gesi yake kutoka Russia.

Muungano huo umeahidi kupunguza utegemezi wake wa mafuta ya Russia kwa asilimia 90 ifikapo mwisho wa 2022, lakini hadi sasa haujatoa ahadi yoyote juu ya gesi.

Marekani imeweka vikwazo dhidi ya bidhaa zote za nishati za Russia kwa lengo la kuiadhibu kwa kuivamia Ukraine.

Hata hivyo, kupanda kwa bei ya mafuta na gesi duniani kunaongeza faida kwa Russia kwa miezi ya hivi karibuni, licha ya kupunguzwa kwa usambazaji wa jumla.

"Kiasi cha mafuta kinapungua katika soko la dunia, bei inapanda," Rais Putin aliambia kundi la wajasiriamali vijana.

**UKRAINE YAPOTEZA WANAJESHI 200 KILA SIKU**

Msaidizi mkuu wa rais wa Ukraine ameambia BBC kuwa kati ya wanajeshi 100 hadi 200 wanauawa vitani kila siku.

Mykhaylo Podolyak, alisema nchi yake inahitaji mamia ya mifumo ya silaha kutoka nchi za Magharibi ili kusawazisha hali ya mapigano katika eneo la mashariki la Donbas.

Pia alisema serikali haiko tayari kuanza tena mazungumzo ya amani na Russia.

Wanajeshi wa Ukraine wanakabiliwa na mashambulizi ya mara kwa mara huku vikosi vya Russia vikijaribu kuchukua udhibiti jimbo lote la Donbas.

"Vikosi vya Russia vimetumia kila aina ya silaha nzito dhidi yetu ikiwa ni pamoja na mifumo mingi ya kurusha roketi na anga," alisema Podolyak.

Alirudia ombi la Ukraine la kutaka silaha zaidi kutoka kwa nchi za Magharibi, akisema kwamba ukosefu kamili wa usawa kati ya majeshi ya Russia na Ukraine ndio sababu ya kiwango kikubwa cha vifo vya wanajeshi wa nchi hiyo.

Ukraine yadai kupiga wanajeshi wa Urusi Kherson

Ukraine imesema jana kuwa imeyapiga maeneo ya jeshi la Russia katika mkoa wa kusini wa Kherson. Wizara ya ulinzi ilisema ndege za kivita za Ukraine zimefanya mashambulizi ya kutokea angani katika maeneo ambako kuna zana za kivita, askari pamoja na maghala katika maeneo matano tofauti ya mkoa wa Kherson.

Katika upande wa mashariki, Ukraine ilisema vikosi vyake vinakabiliwa na mashambulizi makali ya Urusi, wakati vikijitahidi kushikilia ngome zao katika maeneo muhimu ya mji wa Severodonetsk.

Ikiwa Urusi itaukamata mji huo itaweza kuudhibiti ukanda wa Donbas, na pia mto muhimu wa Donets.

**BBC**



Treni ikipita katikati ya soko la mbogamboga katika kijiji cha Tamut Songkhram nchini Thailand. **PICHA: AFP**

# Kenya yapitisha kodi kuku kutoka Uganda

**KAMPALA,** UGANDA

KENYA imeongeza kodi kwa wafanyabiashara wa kuku na mayai kutoka Uganda kwa kuwatoza shilingi 70 za Kenya, sawa na shilingi 2500 za nchi hiyo.

Kulingana na gazeti la Daily Monitor nchini Uganda, ilisema hatua hiyo inakwenda kinyume na makubaliano ya kibiashara kwa nchi za Afrika Mashariki.

Wafanyabiashara na vyama vya wafanyabiashara wameliambia gazeti hilo, kuwa tozo hizo ni miongoni mwa masharti ambayo yamewekwa dhidi ya mayai kutoka Uganda.

Hii inakuja miezi sita baada ya Kenya kuondoa marufuku iliyokuwa imeiweka dhidi ya kuku na bidhaa zake kutoka Uganda kwa ajili ya kuwalinda wakulima wake na athari za Covid-19.

Taarifa ya pamoja iliyotolewa mwezi Januari na Waziri wa kilimo wa Kenya, Peter Munya, Waziri wa biashara Betty Maina, na Waziri wa kilimo wa Uganda Frank Tumwebaze, ilionyesha kuwa Kenya itaruhusu mauzo ya mayai, kuku na vifaranga, baada ya kuzuiwa kuingia nchini Kenya tangu Februari 2021.

**DW**

## Ramaphosa amsimamisha kazi Mkuu wa kupambana na ufisadi

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, amemsimamisha kazi mkuu wa tume ya kupambana na ufisadi nchini humo, Busisiwe Mkhwebane.

Hatua hiyo inachukuliwa wakati bunge likijiandaa kwa vikao vilivyocheleweshwa kwa muda mrefu kutokana na hofu ya kumfungulia mashitaka bungeni.

Mkhwebane aliteuliwa katika wadhifa huo na rais wa zamani Jacob Zuma.

Uteuzi wake ulionekana na wengi kama jaribio la kumlinda Zuma dhidi ya madai ya rushwa.

Kwa miaka mingi, amewasilisha na kupoteza mahakamani msururu wa kesi za kupinga kushitakiwa bungeni.

Bunge ambalo limetawaliwa na chama cha Ramaphosa cha ANC, lilikubaliana mwezi uliopita kuanzisha mchakato wa kumshitaki bungeni.

Taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Rais Ramaphosa mapema jana ilisema Mkhwebane ataendelea kusimamishwa kazi hadi mchakato ulioanza kwenye Bunge utakapokamilika na nafasi yake itashikiliwa na naibu wake.

Ofisi hiyo iliongeza kuwa kutokuwepo kwa Mkhwebane ofisini hakutazuia uchunguzi wowote ambao ulianzishwa naye. Tangazo hilo limekuja ikiwa ni siku moja tu tangu Mkhwebane aanzishe rasmi uchunguzi juu ya Rais Ramaphosa kuficha wizi uliofanyika kwenye nyumba yake ya shambani mwaka 2020.

**DW**

## Trump alaumiwa jaribio la mapinduzi Juni 6

**WASHINGTON,** MAREKANI

JOPO la Bunge la Marekani linalochunguza tukio la uasi kwenye majengo ya bunge uliofanywa Januari 6 mwaka jana, limemtupia lawama rais wa zamani Donald Trump, kwa kupanga mapinduzi.

Katika taarifa yake, jopo hilo lilisema shambulizi hilo halikuwa la ghafla bali lilikuwa ni jaribio la mapinduzi la moja kwa moja la rais huyo kubaki madarakani baada ya kushindwa katika uchaguzi.

Kamati hiyo ya bunge inayofahamika kama kamati ya Januari 6, ilitoa maelezo ya kina yanayoonesha kuwa kauli za mara kwa mara za uwongo alizozitoa Trump kuhusu wizi wa kura na juhudi zake za hadharani za kupinga ushindi wa Joe Biden vilisababisha shambulizi dhidi ya demokrasia ya Marekani.

Mwenyekiti wa kamati hiyo kutoka chama cha Republican Bennie Thompson, alisema demokrasia ya Marekani imebaki hatarini kutokana na njama hiyo ya Trump.

**DW**

# Waziri Mabula aagiza fidia mgodi Nyanzaga

**Na Munir Shemweta, SENGEREMA**

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amemwagiza Mthamini Mkuu wa Serikali, Evelyne Mugasha, kukamilisha uthaminishaji fidia kwenye eneo la mradi wa mgodi wa Nyanzaga.

Mgodi huo uko Sengerema mkoani Mwanza na wananchi wa eneo hilo wameanza kuelewa taratibu za fidia kwenye eneo hilo.

Waziri aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Sota katika kata ya Igalula wilayani Sengerema mkoani Mwanza wakati wa kufuatilia zoezi la kuwahamisha watu na makazi kwenye mgodi wa Nyazaga.

Mgodi wa Nyazaga unaoendeshwa kwa njia ya ubia kati ya Kampuni ya OreCorp Tanzania Limited (84%) na Serikali ya Tanzania (16%) upo kata ya Ngoma kwenye vijiji vya Sota na Nyabila.

Kufunguliwa kwa mgodi huo kunaenda sanjari na zoezi la utwaaji ardhi kwa eneo lote lililoidhinishwa katika leseni ya uchimbaji madini.

Changamoto katika programu ya kuwahamisha watu na makazi katika eneo la mgodi wa Nyanzaga lenye ukubwa wa ekari 5,683 ni wananchi wachache kutoridhika na kiwango kilichoidhinishwa kama malipo ya fidia ya ardhi na uwepo wa wananchi wanaodai kuwa na haki ya umiliki maeneo ya milima.

Hata hivyo, tayari wananchi 1,236 sawa na asilimia 85 wamechukua fomu namba tatu kwa ajili ya kukamilisha taratibu za kulipwa fidia kupisha program ya kuanza kwa mradi wa mgodi wa Nyanzaga na wananchi 216 sawa na asilimia 15 bado hawajachukua fomu hiyo.

Kwa mujibu wa Dk Mabula aliyekwenda kutoa ufafanuzi wa fidia kwa watu wanaotakiwa kuhamishwa katika eneo la mgodi huo, kwa wale wananchi walioKubali kuchukua fomu namba tatu taratibu za kuthaminishwa zitakamilishwa haraka ili waweze kulipwa fidia.



Alisema wale wasiokuwa tayari taratibu za uthamini ziendelee mpaka watakaporidhika.

Dk. Mabula alisema uamuzi wa serikali katika kulipa fidia ya kuwahamisha wananchi wa eneo hilo umezingatia taratibu zote za kisheria zikiwemo za kimataifa na hakuna mtu atakayepunjwa au kukopwa.

"Mthamini Mkuu wa Serikali alifanya mapitio na kuongeza kiasi cha malipo ya fidia ya ardhi hadi milioni mbili kwa ekari moja sambamba na aina ya miti nane kufanyiwa kazi kwa miti mitano kuongezwa katika jedwali, miti mitatu imeongezwa kiasi cha kiwango cha malipo," alisema Dk Mabula.

Waziri aliwaeleza wananchi wa kijiji cha Sota kuwa, tamko la sera ya ardhi linaeleza wazi kuwa maeneo ya milima hayapaswi kumilikiwa na mtu binafsi na zaidi ya Sera maeneo hayo yanapaswa kulindwa hivyo ni maeneo ya umma.

"Kama kuna mtu yeyote anamiliki mlima na mwenye hati tutakuwa tayari kumlipa, maana Sera inaeleza wazi kuwa maeneo ya milima hayapaswi kumilikiwa na mtu ni maeneo nyeti," alisema Dk Mabula.

Aliwatahadharisha wananchi kuhusu maendelezo kwenye eneo la mradi maarufu kama TEGESHA kwa lengo la kutaka kulipwa fidia huku kukiwa na tarehe ya mwisho ya katazo la kufanya maendelezo.

Utegeshaji katika eneo hilo la mradi wa Nyanzaga umefanyika kwenye mazao aina ya alovera, katani, mibono, nanasi na migomba, miti mfano mikalibea na mikaratusi pamoja na utegeshaji wa nyumba mfano ujenzi wa nyumba mpya mahali palipokuwa nyumba ya zamani.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza asingependa kuona migogoro katika maeneo yenye uwekezaji mkubwa unaonufaisha watanzania," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa alisema kuna fursa nyingi zitakazopatikana baada ya mradi mkubwa wa mgodi wa madini ya dhahabu wa Nyanzaga kuanzishwa.

"Fursa zitakazopatikana baada ya mgodi kuanza zitawasaidia wananchi wa kijiji cha Sota na nimpongeze mwekezaji ambaye kabla ya kuanza kazi ameanza kuisaidia jamii ya kijiji hicho hata kabla kuwekeza," alisema.

Alimtaka mwekezaji kuandaa mpango kazi utakaonesha kila mwaka atachangia kiasi gani katika maendeleo ya eneo la mradi huku akibainisha moja ya faida watakayonufaika wananchi wanaoishi eneo la kuzunguka mgodi ni fursa ya ajira.

Moris Omoro, mkazi wa kijiji cha Sota katika kata ya Igalula wilayani Sengerema ambaye ni mlemavu wa miguu alisema bado hajapata uhakika wa ajira kwa watu wenye ulemavu na kuomba mwekezaji wa mgodi kufikiria namna ya kuwapatia ajira pale mgodi utakapofunguliwa.

## DC ahimiza wananchi kupata chanjo corona

**Na Elizabeth John, Njombe.**

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa amewataka wananchi wa kijiji cha Boimanda kata ya Matola kuacha habari za upotoshaji kuhusu matumizi ya chanjo ya UVIKO 19 na badala yake wahamasike kuchanja.

Alitoa rai hiyo katika ziara yake kijijini hapo ambapo alisema wananchi wanapaswa kupuuza habari za mitandaoni zinazodai kuwa chanjo ya UVIKO inasababisha madhara kwenye afya na kusababisha kifo na pungufu wa nguvu za kiume.

"Ingekuwa chanjo ya UVIKO ina madhara basi Mheshimiwa Rais angekuwa wa kwanza kupata madhara hayo kwani ndiye aliyeongoza zoezi la utoaji chanjo. Mimi mwenyewe nimechanja na mpaka sasa bado nipo vizuri na ingekuwa kuuliwa tungeuliwa kwa njia mbalimbali," alisema

"Huduma ya chanjo haijaanza leo ni huduma ya siku nyingi ukiona mtu anaongea maneno ya uongo kuhusu chanjo basi huyo ujue hayajamkuta. Tujitokeze kuchanja chanjo ni salama na ni kwa ajili ya uhai wetu,"alisema Kasongwa.

Wakizungumza mara baada ya kusikiliza elimu ya chanjo waliyopatiwa na Mkuu wa Wilaya baadhi ya wananchi wamesema hawakuwa na elimu sahihi kuhusu chanjo ya Uviko 19.

"Mwanzoni nilikua sielewi maana walisema kuwa chanjo zina madhara na wakati mwingine zinaweza kusababisha kifo lakini nashukuru leo nimepata elimu na nimechanja. Nawashauri wenzangu ambao bado hawajachanja kuhakikisha kuwa wanachanja,"alisema Winifrida Mgaya.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe anaendelea na ziara yake ya kutembelea katika kila kijiji kuzungumza na wananchi na kutatua kero mbalimbali.

# Makalla aagiza usimamizi mkali machinjio Vingunguti

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam Amos Makalla, ameielekeza Halmashauri ya Jiji hilo kumsimamia mkandarasi anayetekeleza mradi wa machinjio ya Vingunguti na kuhakikisha yanakamilika kabla ya Agosti 30 mwaka huu.

Makalla alitoa maelekezo hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati alipotembelea machinjio hayo kwa mara ya nne ili kukagua utekelezaji wake baada ya ukamilikaji wake kusuasua kwa kutolewa ahadi zisizokamilika.

Alisema ziara za Rais Samia Suluhu Hassan alizokuwa akizifanya nje ya nchi zimefungua fursa mbalimbali za biashara ikiwemo ya nyama, hivyo alisisitiza kuwa ni lazima machinjio hiyo ikamilike kwa wakati kwa mustakabali wa soko la nyama la nje ya nchi.

"Ili machinjio yetu yaendane na mahitaji na dhamira ya kisasa jambo muhimu na



kubwa ni kukamilika kwa 'cold room' vyumba vya kuhifadhia nyama na bucha, leo ndiyo ulikuwa msukumo wangu kuja nihakikishiwe kuwa zinakamilika lini na mmeahidi mwezi wa nane kwamba zitakidhi viwango vya kusafirisha nyama," alisema na kuongeza

"Nawaachia jukumu la kumbana mkandarasi, nalisema hili kwa sababu Rais ameenda Dubai amekutana na wafanyabiashara mbalimbali na ziara zake zote kuna watu wanataka kufanya biashara na Tanzania mojawapo ikiwa hii ya nyama uhitaji ni kubwa, lakini nyama zinazochinjwa ziko katika ubora, ziko katika mazingira ya kusafirishwa, tunao uwezo mkubwa wa kuhifadhi, jibu ni machinjio haya," alisema Makalla.

Aliongeza kuwa ni matumaini yake kwamba mkandarasi anaetekeleza mradi huo atafanya kazi usiku na mchana kwa kiwango kinachotakiwa ili watu wasihangaike kufuata nyama Misumgwi, akieleza kuwa wameboresha mnada ili machinjio hiyo ikamilike na watu wapate urahisi.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wa nyama katika machinjia hayo kubadilika kwa kufuata utaratibu watakaopewa wa kufanya biashara kwenye mabucha ambayo yanatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

"Wafanyabiashara lazima tubadilike huwezi ukapikiwa chakula kizuri kinanukia halafu ukapakuliwa kwenye mfuniko wa pipa, chakula hicho hakina ladha, leo mnatengenezewa bucha la kisasa lazima na nyie muendane na usasa, tusifanye biashara kwa mazoea," alisisitiza Makalla.

Pia alisema machinjio hiyo ni kubwa kwani kwa siku inaweza kuchinja Ng'ombe 1,000, Kondoo 500 na Mbuzi 500, akieleza kuwa soko likiendelea kuwa kubwa maisha ya watu wanaozunguka maeneo hayo yatazidi kuimarika zaidi.

Machinjio hiyo imegharimu zaidi ya Sh. Bilioni 15.4 na hadi sasa imekamilika kwa asilimia 97.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# Kama ipo, ipo tu-9




**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani.

Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

****************************************

Kwa upendo wa hali ya juu, wakajikuta wamekumbatiana. Wakakumbatiana kwa muda mrefu huku kila mmoja akitamani kuendelea kuwa na mwenzake, lakini haiwezekani. Baadaye wakakumbuka kuwa wanaitana kaka na dada. Wakaachiana.

"Sasa unaondoka lini?" Akauliza Siwatu kwa sauti ya kichovu kama mtu ambaye ametoka kulia msiba wa wazazi wake wiki nzima.

"Huu ni mchana, kesho asubuhi mimi naondoka. Na siyo kwamba nitaondoka hapa peke yangu. Nataka unisindikize hadi karibu na kijiji cha pili, inatosha sana, nitafarijika sana. Ila nadhani ukibaki peke yako, watakurudisha kwenye kundi hapa kijijini."

"Aka mwenzangu, unafikiri mimi nitawachangamkia kama zamani? Watasubiri sana. Wakinisalimu nitaitikia, lakini mimi niwaanze, hapana. Nitaishi maisha haya nikiendelea kuugulia kuondoka kwako."

"Usijali Siwatu, nimekwambia mimi ipo siku nitarudi tu hapa."

"Usichelewe sana sasa, siyo ukae huko miaka miwili. Hunikuti." Bakari alishtuka.

"Utaenda wapi?"

"Nitakuwa nimekufa kwa simanzi." Akajibu akifuta machozi, jibu hilo lilimfanya Bakari atabasamu.

"Haitofika hata mwaka mmoja, kwa sababu hata mimi siwezi kukaa muda wote huo bila kukuona mkombozi wangu. Hebu kapike ugali bwana tule. Alimyanyua mkono.

Kivivu Siwatu alisimama akielekea nje jikoni kwa ajili ya kutayarisha chakula.

"Bakari unaondoka kweli baba? Umejua kuniliza mwanaume wewe."

********************************

**"Safiri salama swahiba mpenzi, upate neema uendako na heri, ukumbuke nyuma ninayo majonzi, urudi mapema tu uniondoe simanzi." Hayakuwa maneno, bali ni wimbo aliouimba Siwatu akimuimbia Bakari aliyekuwa akiondoka.**

"Safiri salama swahiba mpenzi, upate neema uendako na heri, ukumbuke nyuma ninayo majonzi, urudi mapema tu uniondoe simanzi." Hayakuwa maneno, bali ni wimbo aliouimba Siwatu akimuimbia Bakari aliyekuwa akiondoka.

Aliimba kwa hisia kali mbele ya Bakari na kuwafanya wote watokwe na machozi. Bakari hakujibu kitu, bali alijibu kwa maneno yenye unyeyekevu.

"Safari ni safari swahiba dada yangu Siwatu, huwezi kujua ninapoenda itakuwaje. Lakini kama nitafika salama na maadui zangu hawatonifuata tena kuitoa roho yangu, nitakuja tena. Nitarudi kwa ajili yako mkombozi wangu. Hatua chache kutoka hapa ni sehemu ambayo uliniokoa kutoka kwenye mdomo wa mauti. Ni wewe ndiye mwanamke pekee uliyerudi kunisaidia, huku wenzako wakiondoka bila msaada wowote.

Ndiyo mwanamke ambaye ulinimwagia maji na kunipa mengine ninywe na nikapata nguvu, maana zilikuwa zinaniishia kila sekunde ilipokuwa inayoyoma, leo nikusahau, haiwezekani,"

Maswahiba hao walikuwa wamesimama njiani porini mita chache tu kutoka pale walipoonana kwa mara ya kwanza, Siwatu akiwa na mashoga zake wakitoka kuchota maji, Bakari akiwa nusu mfu.

Ilikuwa ni saa mbili asubuhi, ndege wakiendelea kuimba nyimbo mbalimbali kukaribisha siku mpya.

Waliuangalia kama majogoo wanaotaka kupigana. Waliangaliana kwa muda mrefu. Kila mmoja alikuwa na mawazo yake kichwani. Kuachana na mtu ambaye umezoeana naye. Kuachana na mtu aliyemsapoti kwenye shida zilizotokea. Kuachana na mtu ambaye hakujali kelele za watu wote na vitisho vilivyosemwa, badala yake waliandamana kila wanakokwenda kama vipepeo. Walijikuta wakikumbatiana. Kila mmoja hakutaka hata kumuachia mwenzake. Machozi yalianza kuwatoka wote wawili. Walilia kimya kimya, baadaye wakahamia kwa sauti.

Hakuna aliyetaka kumuachia mwenzake. Baada ya muda mrefu waligundua kuwa watu wanaweza kuwakuta njiani. Wakaachiana. Bakari aligeuka taratibu. Akajikaza kwani aliona akiendelea hivyo wanaweza kukesha wanaangaliana. Akaanza kuvuta hatua taratibu za kuondoka. Hatua zake na jinsi alivyotembea alikuwa kama kondoo anayepelekwa machinjioni. Mwili ulikuwa unaelekea mbele, lakini kichwa kinaangalia nyuma. Alikuwa anamuangalia Siwatu. Alitaka kutamka neno lolote la kumuaga, lakini sasa alijikuta sauti haitoki.

Siwatu aliendelea kusimama katikati ya njia, akimuangalia rafiki yake.

Kila kilichofanyika hapo ni kama vile mke na mume, au mtu na mchumba wake wanaagana. Lakini haikuwa hivyo. Ni mtu na rafiki yake. Ni mtu na mwokozi wake. Ni watu waliolala chini ya paa moja kwa miezi mitatu. Hawakugusana. Mmoja akilala kitandani mmoja analala chini. Ni kama walikuwa wakifanyiana zamu, leo nani alale chini nani kitandani. Lakini hakuna hata mmoja aliyewahi kumtamkia mwenzake chochote kile. Walipendana kama kaka na dada. Na waliitana hivyo.

Ni kama vile kila alivyokuwa anapiga hatua mbele, alikuwa anataka kusimama. Alikuwa akiiangalia sura yenye samanzi na msiba mkubwa. Baadaye aliona kama akiendelea hivyo, anaweza kuahirisha safari yake. Akageuka na kuangalia mbele. Akatikisa kichwa kwa masikitiko. Hatoiona tena sura ya rafiki yake Siwatu na hakujua ni lini au mwaka gani ataiona tena.

Mpaka wakati huo Siwatu alikuwa amesimama pale pale. Aliona kama ni ndoto mbaya ambayo hajawahi kuiona tangu azaliwe.

Alimuangalia Bakari tangu anavuta hatua, mpaka akawa anaishia kwenye miti na majani. Machozi yalimziba macho akawa haoni tena.

*******************************

Ilipita mwezi mmoja baada ya Bakari kuondoka. Siwatu alijiona kama anaishi kwenye kijiji kipya ambacho hakuwahi kuishi kabla.

Nafuu yake ni pale anapolala tu. Akiamka humuwaza Bakari. Hata mwenyewe alianza kujishangaa. Kumuwaza mtu ambaye hajawahi au kupata kuwa mpenzi wake. Hata hivyo alichojua yeye ni mazoea tu.

Pia ni kama wanakijiji walianza kumsuta. Alidhani kuwa baada ya kuondoka Bakari ambaye ndiye aliyesababisha atengwe, basi wanakijiji watamchangamkia kama zamani. Haikuwa hivyo.

Ni wachache tu waliokuwa wakiongea naye. Wengine walimbeza. Wapo waliomcheka.

"Hehee Hooiiii, ulidhani umepata bwana kutoka mbali, ukadharau watu wote kijijini, haya sasa huyoo kaenda kwao, kakuacha hapa hapa kukauka kama kipande cha muhogo." Kuna siku msichana mmoja alimwambia laivu, siyo kwa mafumbo wala nini.

Kwa kawaida alikuwa mpole. Hakutaka kugombana na mtu, hivyo alibaki kimya. Hata ile huruma kuwa mtoto yatima na kupata upendeleo maalum ilianza kupotea.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MASTAA WA ZAMANI WAWATIA MOYO STARS

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa zamani wa timu ya taifa ya Tanzania Taifa Stars, wamewatia moyo wachezaji wa timu hiyo wa sasa, baada ya kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Algeria, Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wachezaji Dua Said aliyeichezea Stars na Simba, pamoja na Juma Pondamali aliyewahi kuichezea timu hiyo, Yanga na Pan African wamewataka wachezaji wa Stars kupambana kwa sababu bado wana nafasi ya kufuzu fainali ya AFCON mwakani nchini Ivory Coast.

"Vijana walijitahidi kadri ya uwezo wao, naweza kusema haikuwa bahati yetu, walitengeneza nafasi nyingi na wakajaribu kuzitumia lakini hazikutinga wavuni, kuna kile kichwa cha mbuzi alichokosa Mbwana Samatta, halafu kuna mashuti mawili aliyopiga Feisal Salum yalikuwa yanababatiza tu wachezaji, wao walipata nafasi mbili wakazitumia, japo lile bao la kwanza kwa mtazamo wangu lilikuwa jepesi sana, lakini isiwavunje moyo, matumaini ya kufuzu bado tunayo," alisema Dua, ambaye enzi zake alicheza kama winga wa kulia, wakati mwingine wa kushoto.

Naye kipa mwenye mbwembwe za zamani za Stars, Pondamali amesema kuwa Stars ilijitahidi, lakini anadhani ilikosa hamasa.

"Sikuona hamasa kwa kikosi chetu, unajua ile amsha amsha na ahadi mbalimbali, zinawafanya wachezaji wacheze juu ya uwezo wao wa kawaida, wajitume kwenye mechi iliyopita sikuiona, lakini bado nafasi ipo na timu ni nzuri," alisema.

Ni matokeo ambayo yaliiwezesha Tanzania kwenye nafasi ya tatu ya msimamo wa Kundi F juu ya Algeria yenye pointi sita, Niger ikiwa kwenye nafasi ya pili kwa pointi mbili na Uganda ipo nafasi ya nne.




Wanafunzi wa shule ya Sekondari Dar es Salaam, wakicheza mpira katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makala kufunga mashindano ya Golf Open 2022

**Na Shufaa Lyimo**

MKUU wa mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala anatarajiwa kufunga mashindano ya TFS Lugalo Golf Open 2022 ambayo yanatarajiwa kuanza Juni 18 hadi 19 mwaka huu kwenye viwanja vya Klabu hiyo, Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo Golf, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo alisema awali mashindano hayo yalipangwa yafanyike Juni 5 mwaka huu, lakini yalisogezwa mbele kutokana na kuingiliana kwa ratiba yao.

"Maandalizi ya mashindano yetu yanaendelea vizuri tunategemea Mkuu wa Mkoa, Amos Makala atatufungia mashindano yetu," alisema Luwongo.

Alisema anaushukuru uongozi wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kuamua kuwa nao bega kwa bega takribani miaka mitatu mfululizo ambapo wamehakikisha mchezo huo unazidi kusonga mbele.

"Tunawashukuru watu wa TFS ambao wamejitahidi kutupambia viwanja vyetu vya golf ambavyo vinaonekana kuwa na ubora wa hali ya juu kutokana na kazi nzuri wanayoifanya," alisema.

Kwa upande wa mwakilishi wa TFS, Anna Lawuo aliwaomba wadau wengine waungane nao kwa ajili ya kuuendeleza mchezo huo.

Naye nahodha wa Klabu hiyo, Japhet Masai alisema kuwa maandalizi yanaendelea vizuri na wanaamini yatafanikiwa kwa kiwango cha juu.

Naye Ofisa masoko wa kampuni ya Serengeti, Faithy Moshy alisema wanaungana na Watanzania kuuendeleza mchezo huo hapa nchini.

## Tembo Warriors dimbani Ulaya leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Tembo Warriors leo kitashuka dimbani nchini Poland na kucheza na timu ya Taifa ya nchi hiyo ambao ni wenyeji wa mashindano ya Ulaya kwa wachezaji wenye ulemavu kwenye uwanja Hutikin Center uliopo jijini Warsaw.

Tembo Warriors ipo nchini Poland kwa ajili ya michuano hiyo ambayo wamealikwa na kutumia kama maandalizi ya kujiandaa na mashindano ya Dunia yatakayofanyika Oktoba mwaka huu, Uturuki.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la soka la watu wenye ulemavu Tanzania, (TAFF), Mosses Mabula alisema wamewasili Poland salama na wanapumzika na leo watakuwa na mchezo wa kwanza ambao watacheza saa 6:00 mchana.

Alisema timu hiyo inaongozwa na Kocha wao, Ivo Mapunda na wachezaji wote wako vizuri na tayari kwa ajili ya kupambana katika mchezo huo dhidi ya wenyeji wao Poland.

"Wachezaji wote wako fiti na kesho (leo) saa 6:00 mchana tutacheza mechi yetu ya kwanza ya ufunguzi dhidi ya Poland ambao ni wenyeji wa mashindano ya Ulaya," alisema Mabula.

Alisema mashindano hayo watayatumia vizuri kwa ajili ya kujiandaa na michuano ya itakayofanyika Uturuki.

## Polisi yapania pointi tatu kwa Namungo

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Polisi Tanzania imepania kuondoka na pointi zote tatu katika mchezo wake wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya Namungo FC utakaopigwa Juni 16 mwaka huu mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha msaidizi wa Klabu hiyo, George Mketo alisema kuwa wanaendelea kuwapa mbinu wachezaji wake ili wapate ushindi ugenini.

"Tunaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu dhidi ya timu ya Namungo ni mchezo ambao utakuwa na upinzani mkubwa," alisema Mketo.

Alisema wamejipanga kupata pointi tatu muhimu katika mchezo wao huo na kudai anaendelea kuyafanyia kazi mapungufu madogo madogo yaliyojitokeza kwenye michezo iliyopita.

Alisema anaiheshimu timu ya Namungo kwani msimu huu hakuna timu ya kuibeza kila timu imejipanga vizuri.

Alisema katika michezo iliyopita alibaini makosa ya kiufundi ambayo anaamini hayawezi kujirudia katika mchezo wao huo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NUNEZ FRESH LIVER
LIVERPOOL imefikia makubaliano binafsi na mshambuliaji wa Benfica mwenye umri wa miaka 22, raia wa Uruguay, Darwin Nunez. ***(The Athletic)***

### CHAMBERLAIN AWANIWA
KLABU ya Manchester United inatafakari uhamisho wa kiungo wa kati wa zamani wa Liverpool, Alex Oxlade-Chamberlain mwenye umri wa miaka 28. ***(TalkSport)***

### ARMSTRONG AWINDWA
KLABU ya Middlesbrough imezungumza na Southampton kuhusu mkataba wa mkopo kwa ajili ya mshambuliaji, Adam Armstrong mwenye umri wa miaka 25. ***(TeamTalk)***

### MANE PAUNI MIL 40
LIVERPOOL wanataka pauni milioni 40 ili kumuachia Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30 ambaye anawaniwa na Bayern Munich. ***(Telegraph)***

### STERLING KUONDOKA CITY
KLABU kubwa za Ulaya zinaamini kuwa Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27, yuko tayari kuondoka Manchester City msimu huu, huku Chelsea ikiwa ni miongoni mwa klabu zinazomtaka. ***(Telegraph)***

### BARCA NA NYOTA
WAKALA Jorge Mendes amezungumza na Barcelona kuhusu upatikanaji wa mshambuliaji wa AC Milan, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 22 na kiungo wa kati, Ruben Neves mwenye miaka 25. ***(Sport)***

### SILVA KUMRITHI DE JONG
BARCELONA wamekuwa katika mazungumzo kumuhusu mchezaji wa Manchester City, Bernardo Silva, lakini wanaweza tu kumsajili kiungo huyo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 27, iwapo watamuuza kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### BOTMAN AGOMBEWA
KLABU ya Paris St-Germain imewasiliana na Lille kuhusu kumtaka Sven Botman baada ya mazungumzo na AC Milan kukwama, ingawa Tottenham Hotspur, Manchester United na Chelsea pia wameulizia kuhusu mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 22, huku Newcastle wakiwa bado wana nia naye. ***(90min)***

### DIABY KUBAKI
BAYER Leverkusen wameiambia Newcastle United kuwa wanapanga kubakia na winga, Moussa Diaby mwenye umri wa miaka 22, hata baada ya msimu huu. ***(Express)***

### GUNDOGAN ANAWINDWA
KIUNGO wa kati wa Manchester City, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 31 ambaye mkataba wake unaendelea hadi mwaka 2023, anatakiwa na Barcelona na Juventus. ***(Bild)***

### KEANE ATAKIWA
KLABU ya West Ham ina nia ya kutaka kumsajili nyota wa Everton, Michael Keane mwenye umri wa miaka 29. ***(Football Insider)***

### GAVI KUBAKI BARCA
LIVERPOOL iko tayari kulipa pauni milioni 42.5 kuondoa kipengele cha mkataba kwa ajili ya kiungo wa kati wa Hispania, Gavi, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 anapenda kubaki Barcelona. ***(La Porteria, via Teamtalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SILVA ANAWEZA KUTUA BARCA

**Asema kwa sasa hawezi kuzungumza lolote kwa sababu yupo na majukumu ya timu ya taifa, lakini...**

**LISBON, Ureno**

BERNARDO Silva hajakataa uwezekano wa kuhamia Barcelona baada ya kuisaidia Ureno kupata ushindi dhidi ya Jamhuri ya Czech kwenye Ligi ya mataifa ya Uefa, juzi.

Kiungo huyo wa kati wa Manchester City amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi Kuu England, lakini kocha wa Barca, Xavi amripotiwa kumuwania atue kule Camp Nou.

Kocha wa City, Pep Guardiola wiki hii alitilia shaka iwapo Barca wanaweza kuwamudu wachezaji kama Robert Lewandowski na Silva takribani mwaka mmoja baada ya kumpoteza Lionel Messi kutokana na matatizo ya kifedha katika klabu hiyo.

Kuhamia Manchester United kwa Frenkie de Jong kunaweza kuwaweka Blaugrana hao kwenye nafasi ya kumnunua Silva.

Silva mwenye umri wa miaka 27, alifunga mabao yote mawili katika ushindi wa Ureno wa 2-0 pale kwenye uwanja wa Jose Alvalade kabla ya kuulizwa kuhusu uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Alisema: "Ikiwa Barcelona watanipa ofa? Kwa bahati mbaya, hivi sasa siwezi kusema chochote. Nipo na timu ya taifa na niko makini sana. Msimu ukiisha tutaona kitakachotokea."

Kocha wa Ureno, Fernando Santos alimsifu Silva baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia Alhamisi.

"Anapokuwa kwenye ubora wake, nina uhakika ni miongoni mwa wachezaji bora 10 duniani," alisema.

"Unapozungumzia masuala haya, anayefunga mabao mengi anaonekana zaidi, lakini kiufundi ni miongoni mwa wachezaji 10 bora duniani."

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,004,0

MECHI KALI

ENGLAND
VERSUS
ITALY

1 | 1.87
X | 3.30
2 | 4.28

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINEZ ATAKIWA KUBAKI INTER MILAN



**MILAN, Italia**

WAKALA wa Lautaro Martinez amesema "hakuna sababu" ya mshambuliaji huyo kuondoka Inter Milan kwa sasa.

Martinez alisaini mkataba mpya na Nerazzurri hadi mwaka 2026, Oktoba mwaka jana, lakini anaendelea kuhusishwa na uhamisho wa kuondoka hapo.

Chelsea, Paris Saint-Germain na Atletico Madrid ni miongoni mwa klabu zinazoripotiwa kutaka kumsajili mshambuliaji huyo wa Argentina.

Majuzi Martinez alisema ana furaha kubaki na wababe hao wa Serie A, na wakala wake, Alejandro Camano, hataraji mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kuhama wakati wa dirisha la uhamisho.


Aliiambia fcinternews.it: "Sina sababu ya kufikiria kuna uwezekano kwamba ataondoka Inter.

"Hakuna aliyetuambia chochote, ukweli ni kwamba, mchezaji anayefunga mabao mengi kwenye ligi ngumu kama ya Italia huwa haonekani, lakini bado kuna mkataba wa miaka minne.

"Yupo sawa, anafuraha, anafurahia timu, klabu, wachezaji wenzake. Hakuna sababu za kuondoka. Tunajua soka ndivyo lilivyo, leo nathibitisha hili na kesho kila kitu kinaweza kubadilika. Lakini leo hali ndiyo niliyoieleza."

Aliongeza: "Sijui kitakachotokea siku za usoni kwa sababu ni soka la kulipwa lina mambo mengi. Lakini kwa Lautaro, kuichezea Inter ni jambo la kupendeza, kama kwa wachezaji wengine wengi ambao wangependa kujiunga na Nerazzurri."

# Liverpool wamalizana na Nunez



**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL wamefikia makubaliano binafsi na mshambuliaji wa Benfica, Darwin Nunez, kwa mujibu wa Athletic.

Bila kujali matokeo, mabadiliko ya kudumu yaliambatana na Liverpool kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ripoti za kuondoka kwa Sadio Mane na kutoridhika kwa Mohamed Salah kuhusu mkataba mpya na hali ya Roberto Firmino msimu huu, kunawafanya Liverpool kuingia sokoni.

Baada ya ujio wa Luis Diaz, Januari, inaonekana nyota mwingine wa Amerika Kusini anatarajiwa kutua Anfield akitokea Ureno.

Wakati ripoti zikionesha kuwa hakuna kilichosainiwa na hakuna makubaliano kati ya klabu hizo mbili, lakini taarifa zinasema kwamba, Liverpool wanakaribia kukamilisha mpango huo.

Majadiliano yanaendelea kuhusiana na mkataba, lakini inaeleweka kuwa mkataba wowote utavunja kiwango cha pauni milioni 85.5.

Kocha Jurgen Klopp anasemekana kuwa anampenda mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 raia wa Uruguay, huku klabu hiyo ikitarajia kuchukua hatua iwapo Sadio Mane ataripotiwa kuondoka na kuelekea Bayern Munich.

## HABARI MICHEZO


055,092/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.11/06/22 | 19:00 | Faroe Islands vs Lithuania | 2.31 | 2.90 | 3.30 |
| 02.11/06/22 | 19:00 | Ireland vs Scotland | 2.27 | 3.05 | 3.20 |
| 03.11/06/22 | 21:30 | Arsenal Sarandi vs Banfield | 2.70 | 3.05 | 2.65 |
| 04.11/06/22 | 21:45 | Montenegro vs Bosnia and Herzegovina | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 05.11/06/22 | 22:00 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 3.05 | 3.35 | 2.20 |
| 06.11/06/22 | 22:00 | Girona vs Tenerife | 2.32 | 3.10 | 3.05 |
| 07.12/06/22 | 00:00 | Sarmiento vs Argentinos Juniors | 3.05 | 3.15 | 2.28 |
| 08.12/06/22 | 01:00 | Cuiaba MT vs Bragantino SP | 2.80 | 3.05 | 2.55 |
| 09.13/06/22 | 01:00 | Tombense MG vs CSA AL | 2.70 | 2.75 | 2.90 |
| 10.12/06/22 | 03:00 | Internacional vs Flamengo | 2.80 | 3.30 | 2.37 |
| 11.12/06/22 | 07:00 | Renofa Yamaguchi vs Fagiano Okayama | 3.05 | 2.95 | 2.44 |
| 12.12/06/22 | 08:00 | Mito Hollyhock vs Montedio Yamagata | 2.60 | 3.10 | 2.65 |
| 13.12/06/22 | 08:00 | Blaublitz Akita vs Omiya Ardija | 2.41 | 3.00 | 3.05 |
| 14.12/06/22 | 19:00 | Colon Santa Fe vs Union Santa Fe | 2.43 | 2.95 | 3.05 |
| 15.12/06/22 | 21:30 | Godoy Cruz vs Racing Club | 2.47 | 3.25 | 2.75 |
| 16.12/06/22 | 22:00 | Vasco da Gama vs Cruzeiro | 2.65 | 2.90 | 2.80 |
| 17.12/06/22 | 22:00 | Sporting Kansas City vs New England Revolution | 2.85 | 3.40 | 2.28 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 11/06/2022

| MUDAVV | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 3534 | Ukraine vs Armenia | 1.23 | 5.66 | 12.13 |
| 17:00 | 3702 | Salpa Salo vs Ilves 2 | 1.53 | 4.42 | 4.52 |
| 17:00 | 3761 | Forde vs Aalesund 2 | 1.99 | 3.63 | 3.09 |
| 17:00 | 3822 | Hudiksvalls FF vs IFK Stocksund | 3.09 | 3.68 | 1.98 |
| 17:00 | 3848 | PK-35 vs KPV Kokkola | 2.12 | 3.34 | 3.04 |
| 17:00 | 3907 | IFK Malmo vs Gais | 6.66 | 4.90 | 1.34 |
| 17:00 | 4225 | Brasil Pelotas RS vs Ypiranga RS | 3.28 | 2.79 | 2.29 |
| 17:00 | 4333 | Grorud IL 2 vs Nordstrand | 2.56 | 4.14 | 2.14 |
| 17:00 | 4831 | Husqvarna FF vs Eskilsminne IF | 2.23 | 3.73 | 2.60 |
| 17:00 | 4902 | Rappe Goif vs IFK Berga | 2.60 | 3.24 | 2.46 |
| 17:00 | 5008 | Ullern vs Kvik Halden | 2.29 | 3.68 | 2.55 |
| 17:00 | 5010 | Hps W vs Pallokerho-35 RY W | 2.45 | 3.59 | 2.42 |
| 17:00 | 5870 | IF Karlstad Fotboll vs Sandvikens IF | 2.14 | 3.54 | 2.85 |
| 18:00 | 1906 | Asker vs Alta IF | 2.30 | 3.78 | 2.50 |
| 18:00 | 2337 | Stal Stalowa Wola vs ZKS Unia Tarnow | 1.78 | 3.54 | 3.93 |
| 18:00 | 3418 | RoPs Rovaniemi vs Vifk Vaasa | 2.27 | 3.75 | 2.70 |
| 18:00 | 4010 | Rana FK vs Tiller IL | 2.14 | 4.31 | 2.50 |
| 18:30 | 3863 | FC Ilves vs Kissat-FC Jazz | 2.35 | 3.83 | 2.42 |
| 18:45 | 1429 | RC Arbaa vs JS Saoura | 3.73 | 3.24 | 1.91 |
| 19:00 | 1696 | HK Kopavogs vs Thor Akureyri | 1.51 | 4.40 | 4.79 |
| 19:00 | 1737 | Faroe Islands vs Lithuania | 2.41 | 3.03 | 3.08 |
| 19:00 | 2199 | Wales U21 vs Netherlands U21 | 8.65 | 4.82 | 1.29 |
| 19:00 | 2474 | Ireland vs Scotland | 2.67 | 2.98 | 2.78 |
| 19:00 | 2725 | FC Gute vs Kvarnsvedens IK | 1.80 | 3.73 | 3.63 |
| 19:00 | 4425 | Vjs vs Kaapo Kaarina | 1.81 | 3.82 | 3.48 |
| 20:11 | 2460 | KP Polonia Warsaw vs Legionovia | 2.06 | 3.38 | 3.14 |
| 21:00 | 1295 | Gibraltar U21 vs Bulgaria U21 | 39.18 | 10.77 | 1.02 |
| 21:00 | 3150 | SAO Jose RS vs Floresta CE | 1.80 | 3.14 | 4.41 |
| 21:00 | 4152 | Instituto Cordoba vs Atletico Rafaela | 1.65 | 3.35 | 5.13 |
| 21:10 | 3325 | Tristan Suarez vs Chacarita Juniors | 2.75 | 3.05 | 2.45 |
| 21:30 | 3389 | CA Tigre vs Barracas Central | 1.49 | 3.93 | 5.70 |
| 21:30 | 3412 | Quilmes vs Chaco For Ever | 2.28 | 2.84 | 3.24 |
| 21:30 | 4249 | Arsenal Sarandi vs Banfield | 2.75 | 2.90 | 2.55 |
| 21:30 | 5749 | Flandria vs Gimnasia Jujuy | 2.24 | 2.99 | 3.13 |
| 21:45 | 1085 | Hungary vs Germany | 6.77 | 4.32 | 1.45 |
| 21:45 | 1143 | Wales vs Belgium | 3.94 | 3.59 | 1.86 |
| 21:45 | 2306 | Luxembourg vs Turkey | 6.85 | 4.44 | 1.43 |
| 21:45 | 2952 | Netherlands vs Poland | 1.38 | 4.76 | 7.49 |
| 21:45 | 2978 | Montenegro vs Bosnia and Herzegovina | 2.94 | 2.99 | 2.53 |
| 21:45 | 4799 | Romania vs Finland | 2.22 | 3.08 | 3.38 |
| 21:45 | 5674 | England vs Italy | 1.87 | 3.30 | 4.28 |
| 22:00 | 4863 | Charlotte FC vs NY Red Bulls | 3.11 | 3.42 | 2.24 |
| 22:00 | 4913 | Girona vs Tenerife | 2.01 | 3.10 | 3.85 |
| 22:30 | 1949 | Corinthians vs Juventude RS | 1.65 | 3.29 | 5.30 |
| 22:30 | 2380 | Ponte Preta vs Londrina PR | 2.11 | 2.85 | 3.63 |
| 22:30 | 4552 | CRB AL vs Vila Nova GO | 2.42 | 2.79 | 3.04 |
| 23:00 | 1885 | Guyana vs Haiti | 3.88 | 3.29 | 1.86 |
| 23:00 | 2700 | Campinense PB vs Manaus Fc/Am | 2.25 | 2.89 | 3.24 |
| 23:00 | 4970 | Virgin Islands, U.s. vs Bonaire | 4.42 | 3.59 | 1.68 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# BOSI WA BRIDGE STARS ATOA SABABU TIMU KUSHUKA DARAJA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIBU wa timu ya Bridge Star, Iddi Saleh amesema kufanya vibaya kwa timu yake hadi kushuka daraja kumetokana na ugeni wa mashindano ya ligi daraja la kwanza Kanda ya Unguja

Timu ya Bridge Star ilipanda daraja kutoka Mkoa wa Kusini Unguja msimu uliopita na kucheza ligi daraja la kwanza msimu huu na imeshuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili, Saleh amesema matokeo mabaya ya timu yake yametokana na ugeni na ushindani mkubwa uliopo katika ligi hiyo inayoshirikisha jumla ya timu 16.

Alisema kuwa katika ligi daraja la kwanza zipo timu zenye uzoefu mkubwa wa kucheza ikilinganishwa na wao hali iliyopelekea kufanya vibaya zaidi katika mzunguko wa kwanza kwa kupokea vichapo mfululizo.

Alisema kuwa licha ya ugumu wa ligi, lakini timu hiyo ilikabiliwa na ukata wa fedha hali iliyopelekea kushindwa kusajili wachezaji wenye uwezo mkubwa wa kuibakisha timu katika daraja hilo na badala yake waliendelea na wachezaji walioipandisha timu.

Aidha alisema timu hiyo itajipanga zaidi msimu ujao ili kuhakikisha inarudi Kanda ikiwa tayari na uzoefu wa kucheza ligi hiyo ambayo inatajwa kama ngumu zaidi katika ligi zote za Unguja.

Bridge Star imecheza jumla ya michezo 28, huku ikishinda , mitatu na kufungwa 16,ikitoka sare 9 na kumaliza nafasi ya pili kutoka chini ikiwa na pointi 18.




Mwanafunzi wa shule ya Sekondari Dar es Salaam, Abuu Issa, akijaribu kufunga goli wakati wa mechi ya mpira wa Kikapu, dhidi ya wanafunzi wa Kibasila katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jan**a. PICHA: JUMANNE JUMA**

# Liwale Sensa Cup kurindima hivi karibuni

**Na Sabato Kasika**

MICHUANO ya kuwania Kombe la Sensa Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, inatarajiwa kutimua vumbi wiki chache zijazo ikishirikisha tarafa tatu za Kibutuka, Makata na Liwale Mjini.

Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judith Nguli alisema, lengo la michuano hiyo ni kutaka kuhamasisha watu kujiandaa kuhesabiwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu.

Mkuu huyo wa wilaya alisema, katika michuano hiyo, mshindi wa kwanza atazawadiwa ng'ombe pamoja na Sh. milioni moja, mshindi wa pili mbuzi na Sh. 700,000 na mshindi wa tatu atazawadiwa kuku, mpira na Sh. 500,000.

"Wananchi wa Liwale wanapenda michezo, hivyo tumeona tutumie fursa hiyo kuhamasisha jamii kujiandaa kujitokeza katika sensa kwa kutumia michezo katika tarafa tatu na kila tarafa itakuwa na mashindano yake," amesema Nguli.

Amefafanua kuwa watapatikana washindi wa kitarafa watakaoingia nusu fainali na kisha fainali itakayofanyika Agosti 21 mwaka huu, na kwamba anaamini kuwa lengo walilokusudia la hamasa ya sensa litatimia. DC Nguli amesema, kabla ya mechi, elimu ya sensa itakuwa inatolewa kwa wale wote watakaokuwa wamefika kushuhudia michuano hiyo, na kwamba wako katika mazungumzo na wadhamini ili kufanikisha michuano hiyo.

"Tunazungumza na benki za NMB, CRDB na wadau mbalimbali, kwa ajili ya kudhamini michuano hii kuanzia mipira jezi na vitu vingine, ili ujumbe wetu wa sensa uwafikie wananchi wote wa Liwale," amesema.

Amesema mipango ya maendeleo na uchumi hutegemea takwimu sahihi na kwamba wilaya hiyo imejipanga kufanya makongamano katika ngazi zote lakini pia wakaona kuna haja ya kuwa na michezo hasa soka.

Michezo
Jumamosi Juni 11, 2022
Nipashe





Silva anaweza kutua Barca



Wachezaji wa timu ya taifa ya Hispania, Gavi (kushoto) na Diego Llorente wakimkaba mshambuliaji wa Uswisi, Breel Embolo wakati wa mchezo baina ya timu hizo kwenye michuano ya Ligi ya Mataifa ya Uefa, uliopigwa juzi kwenye uwanja wa GeneveVenue nchini Uswisi. Hispania ilishinda 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA SC YAMFUATA AZIZ KI IVORY COAST

## Injinia Hersi afunga safari kimyakimya kuhakikisha wanamleta Jangwani, watenga mshahara wa...

**Na Saada Akida**

WAKATI wakiwa katika pilika za uchaguzi Mkuu, uongozi wa klabu ya Yanga umeamua kufunga safari kwenda nchini Ivory Coast kumfuata kiungo wa ASEC Mimosas, Stephan Aziz Ki kwa ajili kumsajili ili aitumikie timu hiyo msimu ujao.

Katika kuhakikisha usajili huo unafanikiwa, Makamu Mwenyekiti wa kamati ya usajili ya Yanga, Injinia Hersi Said ametua nchini Ivory Coast kwa ajili ya kukamilisha dili la nyota huyo.

Kutokana na safari hiyo, Hersi fomu yake ya kuwania nafasi ya urais kwenye Klabu ya Yanga ilirudishwa na mzee Mohammed Msumi, Juni 9 mwaka huu, wakati yeye akiwa kwenye majukumu ya usajili.

Kwa mujibu wa chanzo chetu kutoka ndani ya Yanga, Hersi yupo nchini Ivory Coast kuhakikisha wanamalizana na mchezaji huyo ambaye ametengewa dola elfu 5,000 (sawa na Shilingi 11,650,000) kama mshahara wake wa mwezi.

"Sasa hivi tunafanya usajili kulingana na michuano iliyopo mbele yetu, msimu uliopita hatukufanya vizuri katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na tulitolewa mapema, safari hii hatutaki kurudia makosa hayo ndio maana unaona Hersi ameondoka nchini kwenda kumalizana na Aziz Ki kule nchini Ivory Coast," kilisema chanzo chetu.

Alisema baada ya kufanya mazungumzo na Wakala wa mchezaji huyo alimueleza Hersi kwamba, anatakiwa kukutana na nyota huyo baada ya kumaliza majukumu ya timu yake ya taifa katika mashindano ya kufuzu AFCON.

Wakati huo huo, Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mazingiza alisema msimu huu wamejipanga kuimarisha kikosi chao kwa kufanya usajili mzuri kulingana na mahitaji ya benchi la ufundi linaloongozwa na kocha Nesredine Nabi.

"Kuhusu Fiston Mayele ataendelea kubaki ndani ya Yanga ili kuhakikisha tunafanya usajili kulingana na mashindano yaliyopo mbele yetu," alisema Senzo.

# Simba yamkosa Adebayor, yaahidi kushusha vifaa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imetangaza rasmi kujiondoa kwenye mbio za kumuwania winga hatari wa timu ya US Gendamarie, Victorien Adebayor, badala yake imesema itafanya usajili mkubwa wa wachezaji wenye uwezo zaidi ya mchezaji huyo.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema ni kweli klabu hiyo ilikuwa na mipango ya kutaka kumsajili, lakini dili lake limeshindikana baada ya kuwa na vita kali na klabu zingine kubwa.

"Ni vizuri kuliweka hili sawa ili kila Mwanasimba alielewe tusiendelee kujipa matumaini. Ni kwamba dili lake limeshindikana kwa sababu kulikuwa na vita kubwa ya usajili, klabu zingine ziliingilia kati na kuweka 'mzigo' mkubwa tukaamua kuondoka kwenye mbio kwa sababu huwezi kumsajili mchezaji mmoja kwa pesa ya kusajili wachezaji watatu. Kila klabu ina ukomo wake kwenye bajeti yake ya usajili kwa hiyo wanachama na mashabiki wa Simba waelewe kuwa Adebayor si sehemu ya Simba kwenye mipango yake," alisema Ahmed.

Pamoja na kumkosa mchezaji huyo, Meneja huyo alisema kuwa klabu hiyo itafanya usajili mkubwa wa wachezaji wenye uwezo zaidi ya Adebayor kwani ina watu madhubuti na makini wenye uzoefu wa soka la Kiafrika, wenye uwezo wa kupata mchezaji bora kutoka eneo lolote kwenye bara hili au nje ya Afrika.

"Nathibitisha hili kwa sababu wachezaji wengi wazuri kutoka nje ya nchi waliocheza soka la kulipwa Tanzania wameichezea Simba, hii inadhihirisha kuwa ina watu makini kwenye usajili. Unajua wachezaji aina ya Adebayor wapo wengi sana Afrika, ila wengi wanamfahamu huyo kwa sababu timu aliyokuwepo ilikuwa kundi moja na timu yetu kwenye Kombe la Shirikisho kwa hiyo Watanzania wengi walikuwa wanamuona kwenye mechi mbalimbali kwa sababu walikuwa wanazifuatilia, lakini US Gendamarie isingekuwa kundi moja na sisi, sidhani kama wangemjua. Lakini Afrika hii ina wachezaji wazuri zaidi yake, ambao Simba inawawinda kwa sasa," alisema.

Taarifa zinasema kuwa mchezaji huyo tayari amemalizana na RS Berkane ya Morocco ambao ni Mabingwa wa Kombe la Shirikisho iliyokuwa kundi moja na Simba pamoja na US Gendamarie ya Niger aliyokuwa akiichezea winga huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002